Nipashe
Jumatano Julai 1, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580272
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US


Albinism Hotline
• Jifunze kuhusu Ualbino
• Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino
0800 75 00 50
Piga simu bure
HAKI YETU PROJECT
UNDER THE SAME SUN
215779502



## EWURA yatangaza bei mpya mafuta, petroli yapanda

UKURASA 3

# CCM: Wagombea ruksa kujipitisha



• **JPM** aanika sababu kuwania tena, akerwa wasaka urais Zanzibar kuchafuana...*Endelea ukurasa 2*






## BAA LA CORONA

**Utafiti unaonyesha kuwa watoto na vijana wanaweza kupata maambukizi ya virusi vya corona na kuambukiza wengine kama yalivyo makundi mengine. WHO**

- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## Wanne wauawa uvamizi mgodini

UKURASA 3



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store



## Zitto amkaribisha Membe upinzani

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA, AZAM FC ZAIDI YA HESHIMA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# CCM: Wagombea ruksa kujipitisha

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimefungua pazia kwa wanaotaka kuwania nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani kuanza kujipitisha kwenye maeneo wanayotaka kugombea kuanzia leo, lakini kipenga rasmi cha uchukuaji fomu kitapulizwa Julai 14 mwaka huu.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa chama hicho, Rais John Magufuli amewataka wanachama wenzake kutotumia kipindi hicho cha kampeni kukibomoa chama chao, akisisitiza kuwa wavumilivu.

Akizungumza na wanachama wa CCM waliojitokeza alipokuwa akirejesha fomu za kuwania urais kupitia chama hicho jijini Dodoma jana, Rais Magufuli alisema kuanzia leo, wanaCCM ruksa kupitapita kwenye maeneo.

"Ninawaomba wanaCCM kwa upendo mkubwa sana, wale tutakaojitokeza kuwania nafasi mbalimbali za udiwani, ubunge, uwakilishi, tufanye hizi kazi kwa ustaarabu, tukatangulize maslahi ya Tanzania yetu, maslahi pia ya chama chetu.

"Katika kipindi hiki cha kampeni, wanaCCM kamwe tusikitumie kama kipindi cha kukibomoa chama, kwa sababu tutakwenda kule tutaanza kubomoana wenyewe kwa wenyewe.

"Wakati utakapofika sasa wa uchaguzi na kugombea na vyama vingine tutakuwa tumeshajiumiza. Niwaombe sana wanaCCM tukawe wavumilivu, ninaambiwa majimbo mengine kuna watia nia hadi 25, mtarogana bure, mtaumizana bure atakayechaguliwa Mungu anamjua.

"Tuvumiliane, tuheshimiane, tupendane na baada ya uchaguzi, huyo atakayekuwa amechaguliwa, ndiyo tumbebe kwa nguvu zote," aliagiza.

Pia aliviomba vyama vingine vya siasa kuwateua wanawake, vijana na wazee kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

"Tanzania ina umuhimu zaidi kuliko mengine, na ninataka niwathibitishie mambo yanakwenda vizuri, vizuri sana na kila mahali ukigusa, unaona kuna miradi inafanyika.. Hatujali hawa hawakutuchagua, tuliamini kila Mtanzania anahitaji maendeleo," alisema.

AREJESHA FOMU

Dk. Magufuli alisema Juni 17, mwaka huu, alichukua fomu na alitaka uchukuaji wake uwe wa kawaida akifafanua: "Niliamini kabisa uchukuaji fomu wangu uwe kama kawaida yangu, nilijitahidi kuwatoroka vizuri sana, Katibu Mkuu alikuwa ananiuliza nitakuja lini, alipanga na saa tano na saa sita mimi nikaja saa mbili nikachukua fomu nikaondoka.

"Lakini, nilifika jana Katibu Mkuu, Makamu Mwenyekiti na viongozi wengine wamekuwa wakiniuliza unarudisha lini fomu uliyoijaza, ndiyo maana leo nimerudisha fomu, kwa kutambua kwamba mimi ni mtumishi wenu, na inawezekana bado mnanihitaji nitumike,"alisema.

"Ninaomba radhi kwa waliotaka kunidhamini, lakini karatasi hazikutosha, dhamana yao sasa waiweke katika kura zao na kwa wanachama wengine wa vyama vyote, ikiwa nitapitishwa na mikutano inayohusika kuwa mgombea wa urais," alisema.

Katibu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, alisema wanachama 1,023,111 wamejitokeza kumdhamini Dk. Magufuli kuwania urais kupitia chama hicho.

Alisema uchukuaji na urejeshaji wa fomu za urais wa Tanzania na Zanzibar ulitarajiwa kufungwa rasmi jana saa 10 jioni na kuthibitisha kupokea fomu za Rais ambazo zimejazwa vizuri na amekamilisha taratibu za kuomba nafasi hiyo.

"Julai 11, mwaka huu kutakuwa na mkutano utafanyika Dodoma ili kupiga kura kwa mgombea urais wa Tanzania kupitia CCM, ili ateuliwe rasmi na kwa Zanzibar Julai 10 Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) itampigia kura na kuchagua mgombea urais mmoja wa CCM," alisema. Alisema kuanzia leo nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani zipo wazi, hivyo wanachama walio na sifa, waanze kupita kwenye ofisi za wakurugenzi wa uchaguzi kuulizia utaratibu na siyo kuanza kampeni.

"Kwa wagombea nafasi hizo Julai 14 hadi 17 watachukua na kurejesha fomu. Kwa hiyo, hicho kipindi cha kuanzia kesho (leo) ni cha kujipitishapitisha na siyo cha kufanya kampeni.

"Atakayekiuka kanuni, Mzee Mangula yupo hapa na mimi nipo nyuma yake, tunahitaji ushindani wenye utulivu, wa kistaarabu, wa kiCCM na matarajio tutapata wagombea wazuri wa kushindana na vyama vingine," alisema.

## JPM ataja sababu za kugombea tena

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, amewanyooshea kidole wagombea wa urais Zanzibar kupitia chama hicho, ambao wameanza kuchafuana mitandaoni, huku akiwataka kunadi sera zao kwa uangalifu.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wanachama wa CCM na viongozi mbalimbali baada ya kurejesha fomu ya kuwania Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili.

Alisema wagombea hao watambue kuwa atakayechaguliwa ni mmoja na Mungu ndiye anayemjua.

"Naomba wana CCM tuwe wavumilivu nimeanza kuiona dalili kwa wagombea 33 Zanzibar, wengine wanatumia mitandao wanamsema mwenzao wengine kwenye magazeti, lakini atakayechaguliwa ni mmoja tu na Mungu wetu wa mbinguni anamfahamu, sisi tulikuwa 42," alisema.

Aliwaomba wagombea hao kuwa waangalifu katika kunadi sera zao wasiumizane kwa kuwa wanatoa nafasi kwa washindani wao.

"Tunawapa nafasi washindani wetu, kazi sio urais tu...wenyeviti wangu wa mikoa wote hapa mlikuwa na uwezo wa kuwa marais, lakini mkasema nenda Magufuli tukutume, naambiwa majimbo mengine kuna watia nia hadi 25 mtarogana bure, mtaumizana bure atakayechaguliwa Mungu anamjua," alisema.

"Niwaombe wanachama tusivunje umoja wetu tukigombana sana wakati wa kampeni hizi zitatupotezea direction (mwelekeo), tuvumiliane, tuheshimiane tupendane na baada ya chaguzi huyo atakayekuwa amechaguliwa ndio tumbebe kwa nguvu zote," alisema.

Alieleza kuwa nafasi zipo nyingi na ana nafasi nne ambazo anatakiwa kuteua anashindwa kuelewa amteue nani.

**KILICHOMSUKUMA KUCHUKUA FOMU**

Alibainisha kuwa kilichomsukuma kuchukua fomu kuomba kuwania urais kupitia chama hicho ni kutokana na mipango mbalimbali ambayo haijakamilika na hakuamini kama atatokea mwingine kuikamilisha vizuri.

"Hichi ndicho kilichonifanya kuchukua fomu, sikutaka kuwa mbinafsi kwa kuwa si mimi tu ndio nastahili kutawala, sio mimi tu nastahili kuongoza niliona changamoto ambazo zipo."

Alisema bado kuna changamoto nyingi nchini huku akisema yale yaliyopangwa kutekelezwa na serikali ya awamu ya tano kwa kipindi cha miaka mitano mipango mingi imetekelezwa na ambayo haikupangwa.

"Naomba nikiri kwenu wakati tunatekeleza mipango hii tumegundua kuna mipango mingi inahitaji kutekelezwa na mingine imeanza kutekelezwa haijakamilika kama SGR tumetumia Sh. trilioni 7.025 kujenga na inafika Makutupora na inatakiwa ifike hadi Mwanza na Kigoma na sehemu nyingine," alisema.

Pia alisema upo mpango wa umeme wa bwawa la Mwalimu Nyerere (Stigles gorge) ambao unagharimu Sh. trilioni 6.5 na utawezesha kuzalisha umeme megawati 2,115.

"Kingine katika historia ya nchi yetu tulipoingia madarakani tulikuwa na vijiji vyenye umeme 2132 leo tuna vijiji 9114, bado vijiji 3,000 ili Tanzania kila kijiji kiwe na umeme, kwa hiyo mpango tumeuanza bado hatujaukamilisha.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, akikagua fomu za mgombea pekee wa urais aliyeomba kupitia chama hicho ambaye ni Rais na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Dk. John Magufuli, kabla ya kuzipokea katika Ofisi za Makao Makuu jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Zitto amkaribisha Membe upinzani

**Na Mwandishi Wetu, KILWA**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema sasa ni wakati mwafaka kwa Benard Membe kujiunga na vyama vya upinzani.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kilwa mkoani Lindi jana, Zitto alisema mwanasiasa huyo aliyewahi kuwa mbunge na waziri wa wizara nyeti nchini, ana fursa ya kuunganisha Watanzania wenye kiu ya mabadiliko kupitia vyama mbadala vya siasa.

"Ndugu yangu Benard Membe kafukuzwa uanachama wa CCM. Ninajua bado anatetea haki yake ya uanachama huko. Ni hatua sahihi.

"Hata hivyo, muda wa kuleta mabadiliko katika nchi umewadia, ninamsihi afanye uamuzi wa kuunganisha nguvu kupitia vyama mbadala, ili kuwapa Watanzania mabadiliko wanayoyataka," alisema. Zitto ambaye yuko katika ziara ya kichama ya mikutano ya ndani Kusini mwa Tanzania, alisema anaelewa mwanasiasa huyo bado anapambana kubaki ndani ya CCM, lakini muda huu anahitajika zaidi upinzani.

Membe, mmoja wa wanasiasa mashuhuri nchini, alifukuzwa uanachama wake CCM miezi michache iliyopita na hali yake kwa sasa iko kwenye sintofahamu.

Wiki iliyopita, Membe alikaririwa akisema kuwa, ingawa kwa sasa bado anaangalia hatma yake ndani ya CCM, upo uwezekano wa kuwania urais kupitia vyama vingine mbadala.

Hata hivyo, katika mkutano huo wa Kilwa, Zitto alisema historia itamhukumu vibaya mwanasiasa huyo endapo hatafanya uamuzi wa kujiunga na upinzani kwa sasa.

"Mimi ninajua Membe anaipenda Tanzania na ni mwana demokrasia. Adhihirishe mapenzi yake kwa nchi yetu kwa kuongeza nguvu wa vyama mbadala.

"Kama kuna kosa la uhaini, basi itakuwa ni kwa Membe kutofanya uamuzi wa kuwatumikia Watanzania nje ya CCM. Ninamsihi kuwa afanye tafakari na kufanya uamuzi sahihi na wananchi," alisema Zitto huku akishangiliwa na umati uliohudhuria mkutano huo.

HABARI KITAIFA

# Bei ya petroli, dizeli yapaa

Na Mwandishi wetu

MAMLAKA ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetangaza bei elekezi ya mafuta ya petroli na diseli ambayo imepanda kwa kati ya Sh. 170 hadi 173.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na EWURA, bei ya petroli itapanda kutoka Sh. 1,520 hadi 1,693 kwa jiji la Dar es Salaam.

Aidha, diseli itapanda kutoka Sh. 1,546 hadi 1,716 kwa Dar es Salaam, huku Arusha ikiwa ni Sh. 1,711 kwa petroli na Sh. 1,750 kwa dizeli.

Kwa jiji la Dodoma petroli itauzwa Sh. 1,752 na dizeli Sh. 1,775, jijini Mwanza ikiwa ni Sh. 1,843 na dizeli Sh. 1,718.

Mtwara petroli itauzwa kwa Sh. 1,765 na dizeli Sh. 1,640.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, wauzaji wa jumla kwa Dar es Salaam lita moja itauzwa Sh. 1,568.35 na dizeli Sh. 1,591 huku Tanga ikiwa ni Sh. 1,529.75 kwa petroli na Sh. 1,568.28 kwa diseli.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (kushoto), akiangalia ng'ombe wanaofugwa na Gereza la Mifugo Ubena, Bwawani, Mkoa wa Pwani, jana. Wa pili kulia ni Mkuu wa Gereza la Mifugo Ubena, ACP Daimu Mmolosha. **PICHA: WMNN**

# Wanne wauawa kwa mapanga mgodini

Na Shaban Njia, KAHAMA

WAFANYAKAZI wanne wa kiwanda cha uchenjuaji madini ya dhahabu (Plant) katika mgodi mdogo wa Ntambalale, kijiji cha Wisolele, wilayani Kahama wameuawa kwa kucharangwa na mapanga na watu wasiojulikana na kutokomea.

Mwenyekiti wa mgodi huo, Hamisi Mabubu, akiongea na Nipashe kwa njia ya simu, alisema tukio hilo limetokea saa tisa usiku wa kuamkia jana katika moja ya kiwanda cha uchenjuaji wa madini mgodini hapo.

Alisema, wafanyakazi watano wa kiwanda hicho, walivamiwa na kucharangwa mapanga na watu wasiojulikana na kuibia kaboni, huku wanne kati ya hao wakipoteza maisha papo hapo na mmoja Evvary Mbuya, akijeruhiwa.

Mabubu alisema, chanzo cha tukio hilo ni tamaa ya kupata mali kwa haraka, na kudai mwanzo wa mwezi huu pia kulitokea uvamizi kwenye kiwanda cha uchenjauji wa madini na kuiba kaboni, lakini hakukujeruhi mtu.

Diwani wa Kata ya Segese, Joseph Mayala, alisema alipata taarifa ya tukio hilo kutoka kwa mtendaji wake wa kata majira ya saa 10 usiku na walipofika kwenye tukio walikuta miili ya wafanyakazi wa kiwanda hicho ikiwa imehifadhiwa kwenye chumba kimoja cha kiwanda hicho.

Alisema, wakiwa katika harakati za kuwaondoa katika chumba hicho, waligundua mmoja wao ambaye ni Mbuya akiwa bado hai na kumkimbiza Hospitali ya Halmashauri ya mji wa Kahama kwa ajili ya matibabu zaidi.

Mayala alisema, tukio la uvamizi wa kiwanda cha uchenjuaji wa dhahabu sio la kwanza, na hutokea wakati wamiliki wa viwanda wakiwa na kaboni na kuliomba Jeshi la Polisi kuongeza ulinzi na kudhibiti majanga hayo yasiendelee kutokea.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, ACP Joseph Paul, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na harakati za kuwatafuta na kuwatia nguvuni walitotenda tukio hilo zinaendelea ili wafikishwe katika vyombo vya sheria.

# Waziri afichua magari ya Jeshi kusajiliwa kwa namba binafsi

Na Beatrice Shayo

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amefanya ziara ya kushtukiza katika Shule ya Sekondari Bwawani ambayo inamilikiwa na Jeshi la Magereza na kubaini madudu ikiwamo magari ya Jeshi kusajiliwa kwa namba binafsi.

Waziri Simbachawene alianza ziara hiyo jana kwa kutembelea Gereza la Kilimo Ubena na baadaye kuelekea katika shule hiyo ambazo zote zipo jirani ndani ya Kata ya Bwawani mkoani Pwani.

Akizungumza na uongozi wa shule hiyo, Simbachawene alisema Sekondari hiyo ni mali ya umma lazima mali za shule hizo zisajiliwe kwa namba za Jeshi la Magereza zinazojulikana kwa kifupisho cha MT (Magereza Tanzania).

Alisema haiwezekani magari matatu ikiwamo ya Mkuu wa Shule hiyo iwe imesajiliwa kwa namba binafsi, lori pamoja na gari lingine mali ya shule hiyo, kitendo hicho ni uvunjifu wa taratibu za serikali na anahitaji kupewa taarifa ya maandishi.

"Mkuu wa Gereza Ubena wewe ndio kiongozi hapa, nakuagiza umfikishie ujumbe CGP (Kamishna Jenerali wa Magereza), ifikapo kesho (leo) mchana nipate taarifa ya shule hii ikiwemo kwanini magari ya Jeshi yamesajiliwa kwa namba 'private' (binafsi), na pia nipate CV za walimu wa shule hii pamoja na watumishi wote," alisema Simbachawene.

Aliongeza: "Inawezekana shule hii ikawa ni kijiwe fulani ambacho watu wanajipatia fedha, mpaka magari wanasajili kwa namba private ili wafanyie nini?"

" Gari la serikali tunajua hata kama litakuwa linasomba mawe, lakini sio ajabu hiyo gari inafanya kibarua huko mtaani inafanya vibarua vya watu, inabeba matofali, unaitofautisha vipi na magari mengine, siwezi kuhukumu moja kwa moja naomba nipate taarifa ya maandishi kutoka kwa CGP kupitia kwako."

Waziri Simbachawene kutokana na upungufu huo aliyouona, alitaka kujua zaidi ufaulu wa wanafunzi wanaomaliza masomo yao, pia alitaka kujua mapato na matumizi ya shule hiyo ambayo amesema ina mazingira mazuri, eneo zuri, lakini uongozi umeshindwa kuitangaza na haina umaarufu wowote hapa nchini.

Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Solomon Mwambingu, alisema shule hiyo ilianzishwa mwaka 1981, na kuhusu ufaulu inafanya vizuri kuanzia kidato cha nne hadi cha sita.

"Shule inafanya vizuri kitaaluma, matokeo ya kidato cha pili kwa mwaka jana 2019 wanafunzi wote walifaulu, pia kidato cha nne walifanya vizuri na matokeo ya kidato cha sita wanafunzi wote walifaulu na hakukua na daraja sifuri wala daraja la nne," alisema Mwambingu.

Aidha, Waziri Simbachawene kwa upande wa Gereza la Mifugo aliwapongeza kwa kutunza mifugo iliyopo katika gereza hilo, na kuwataka kuwapo na soko la nyama kwa kuchinja ng'ombe ili waweze kuuza na kupata mapato kupitia ufugaji wa kuvuna.

"Lazima magereza ijitegemee, gereza la mifugo halina hata nyama za kuuza, tunataka uchungaji wenye faida, kuwepo na 'brandy' yenu, mnaweza mkachukua mfuko mkaweka nyama na kuandika bwawani meat, na pia kuzalisha maziwa yakutosha, hivyo ndivyo kujitangaza," alisema Simbachawene.

Kwa upande wake Msimamizi wa Shamba la Magereza katika Gereza hilo, Charles Masuka, alisema shamba hilo lina ekari 12 ambapo wanafuga ngombe, mbuzi, kondoo na bata, hivyo shamba hilo linatoa ngombe wa nyama ambapo wanatoa kwa wahitaji.

## TANGAZO

Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

***KUMB: PPR/2020 - 07/1***

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 1 JULAI 2020

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, Tarehe 1 Julai 2020. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja za mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyopokelewa nchini kupitia **bandari ya Dar es Salaam** zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Juni 2020. Bei za Mafuta ya Taa zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo lililopita la tarehe 3 Juni 2020 kwani hakuna shehena ya mafuta hayo iliyopokelewa mwezi Juni 2020 kupitia bandari ya Dar es Salaam. Kwa mwezi Julai 2020, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 173/lita (sawa na asilimia 11.38) na Shilingi 170/lita (sawa na asilimia 10.98), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 172.39/lita (sawa na asilimia 12.35) na Shilingi 169.22/lita (sawa na asilimia 11.90), mtawalia.

(b) Kwa mwezi Julai 2020, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) hazina mabadiliko na zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo lililopita la tarehe 3 Juni 2020. Hii ni kwasababu, kwa mwezi Juni 2020, hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga.

(c) Hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Mtwara katika mwezi Juni 2020. Hivyo, kwa mwezi Julai 2020, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Dizeli kwa **Mikoa ya Kusini (yaani Mtwara, Lindi na Ruvuma)** hazitabadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Juni 2020. Kutokana na upungufu wa mafuta ya petroli katika maghala ya mafuta mkoani Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es salaam na hivyo bei za rejareja za Petroli kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es salaam pamoja na gharama za usafirishaji wa mafuta hayo hadi mikoa husika. Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

(d) Mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani yanatokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (BPS Premium) kama inavyoonekana katika **Jedwali C na Jedwali D.**

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (formula) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 74 la tarehe 7 Februari 2020.

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

## JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| **Dar es Salaam** | **1,693** | **1,716** | **1,568** |
| **Arusha** | **1,711** | **1,750** | **2,044** |
| Arumeru (Usa River) | 1,711 | 1,750 | 2,044 |
| Karatu | 1,729 | 1,768 | 2,062 |
| Longido | 1,722 | 1,761 | 2,055 |
| Monduli | 1,716 | 1,755 | 2,049 |
| Monduli-Makuyuni | 1,721 | 1,760 | 2,054 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 1,795 | 1,834 | 2,128 |
| **Pwani (Kibaha)** | **1,697** | **1,721** | **1,572** |
| Bagamoyo | 1,704 | 1,727 | 1,579 |
| Bagamoyo (Miono) | 1,735 | 1,758 | 1,610 |
| Chalinze Junction | 1,707 | 1,730 | 1,582 |
| Chalinze (Msata) | 1,711 | 1,734 | 1,586 |
| Kibiti | 1,713 | 1,737 | 1,588 |
| Kisarawe | 1,700 | 1,723 | 1,575 |
| Mkuranga | 1,702 | 1,726 | 1,578 |
| Rufiji | 1,720 | 1,744 | 1,595 |
| **Dodoma** | **1,752** | **1,775** | **1,627** |
| Bahi | 1,759 | 1,782 | 1,634 |
| Chamwino | 1,747 | 1,770 | 1,622 |
| Chemba | 1,778 | 1,801 | 1,653 |
| Kondoa | 1,784 | 1,808 | 1,659 |
| Kongwa | 1,749 | 1,772 | 1,624 |
| Mpwapwa | 1,753 | 1,776 | 1,628 |
| Mtera (Makatopora) | 1,770 | 1,794 | 1,646 |
| **Geita** | **1,858** | **1,882** | **1,733** |
| Bukombe | 1,847 | 1,871 | 1,722 |
| Chato | 1,879 | 1,903 | 1,754 |
| Mbogwe | 1,896 | 1,920 | 1,771 |
| Nyang'hwale | 1,873 | 1,897 | 1,748 |
| **Iringa** | **1,757** | **1,780** | **1,632** |
| Ismani | 1,762 | 1,785 | 1,637 |
| Kilolo | 1,761 | 1,785 | 1,636 |
| Mufindi (Mafinga) | 1,767 | 1,790 | 1,642 |
| Mufindi (Igowole) | 1,776 | 1,799 | 1,651 |
| **Kagera (Bukoba)** | **1,908** | **1,932** | **1,783** |
| Biharamulo | 1,883 | 1,906 | 1,758 |
| Karagwe (Kayanga) | 1,925 | 1,948 | 1,800 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 1,930 | 1,954 | 1,806 |
| Muleba | 1,908 | 1,932 | 1,783 |
| Ngara | 1,896 | 1,919 | 1,771 |
| Misenyi | 1,917 | 1,940 | 1,792 |
| **Katavi (Mpanda)** | 1,901 | 1,924 | 1,776 |
| Mlele (Inyonga) | 1,920 | 1,943 | 1,795 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 1,894 | 1,917 | 1,769 |
| Tanganyika (Ikola) | 1,919 | 1,942 | 1,794 |
| **Kigoma** | **1,924** | **1,948** | **1,799** |
| Uvinza (Lugufu) | 1,936 | 1,960 | 1,812 |
| Buhigwe | 1,913 | 1,937 | 1,788 |
| Kakonko | 1,881 | 1,905 | 1,756 |
| Kasulu | 1,910 | 1,934 | 1,785 |
| Kibondo | 1,888 | 1,912 | 1,764 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **1,700** | **1,739** | **2,033** |
| Hai (Bomang'ombe) | 1,704 | 1,743 | 2,037 |
| Mwanga | 1,693 | 1,732 | 2,027 |
| Rombo (Mkuu) | 1,717 | 1,756 | 2,050 |
| Same | 1,687 | 1,726 | 2,020 |
| Siha (Sanya Juu) | 1,707 | 1,746 | 2,040 |

# TANGAZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Lindi** | **1,752** | **1,745** | **1,627** |
| Lindi-Mtama | 1,770 | 1,749 | 1,645 |
| Kilwa Masoko | 1,727 | 1,768 | 1,602 |
| Liwale | 1,773 | 1,780 | 1,648 |
| Nachingwea | 1,781 | 1,764 | 1,656 |
| Ruangwa | 1,783 | 1,771 | 1,658 |
| **Manyara (Babati)** | **1,745** | **1,784** | **2,078** |
| Hanang (Katesh) | 1,755 | 1,794 | 2,088 |
| Kiteto (Kibaya) | 1,760 | 1,799 | 2,093 |
| Mbulu | 1,758 | 1,797 | 2,091 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 1,777 | 1,816 | 2,110 |
| **Mara (Musoma)** | **1,871** | **1,895** | **1,746** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 1,912 | 1,935 | 1,787 |
| Rorya (Ingirijuu) | 1,880 | 1,904 | 1,755 |
| Rorya (Shirati) | 1,915 | 1,938 | 1,790 |
| Bunda | 1,862 | 1,886 | 1,738 |
| Bunda (Kisorya) | 1,872 | 1,895 | 1,747 |
| Butiama | 1,868 | 1,892 | 1,743 |
| Serengeti (Mugumu) | 1,917 | 1,940 | 1,792 |
| Tarime | 1,882 | 1,906 | 1,758 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 1,887 | 1,910 | 1,762 |
| **Mbeya** | **1,800** | **1,823** | **1,675** |
| Chunya | 1,809 | 1,833 | 1,685 |
| Chunya (Makongolosi) | 1,824 | 1,847 | 1,699 |
| Kyela | 1,816 | 1,839 | 1,691 |
| Mbarali (Rujewa) | 1,784 | 1,807 | 1,659 |
| Rungwe (Tukuyu) | 1,809 | 1,832 | 1,684 |
| **Morogoro** | **1,718** | **1,741** | **1,593** |
| Mikumi | 1,733 | 1,757 | 1,608 |
| Kilombero (Ifakara) | 1,756 | 1,779 | 1,631 |
| Kilombero (Mlimba) | 1,778 | 1,801 | 1,653 |
| Kilombero (Mngeta) | 1,767 | 1,791 | 1,642 |
| Ulanga (Mahenge) | 1,766 | 1,790 | 1,641 |
| Malinyi | 1,777 | 1,800 | 1,652 |
| Kilosa | 1,736 | 1,760 | 1,611 |
| Gairo | 1,736 | 1,760 | 1,611 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 1,728 | 1,752 | 1,603 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 1,718 | 1,741 | 1,593 |
| Turiani | 1,743 | 1,766 | 1,618 |
| **Mtwara** | **1,765** | **1,731** | **1,640** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 1,814 | 1,767 | 1,689 |
| Masasi | 1,791 | 1,747 | 1,666 |
| Newala | 1,797 | 1,752 | 1,672 |
| Tandahimba | 1,790 | 1,745 | 1,665 |
| Nanyamba | 1,790 | 1,745 | 1,665 |
| **Mwanza** | **1,843** | **1,866** | **1,718** |
| Kwimba | 1,861 | 1,884 | 1,736 |
| Magu | 1,851 | 1,874 | 1,726 |
| Misungwi | 1,837 | 1,861 | 1,712 |
| Sengerema | 1,875 | 1,899 | 1,750 |
| Ukerewe | 1,902 | 1,926 | 1,778 |
| **Njombe** | **1,785** | **1,809** | **1,660** |
| Njombe (Kidegembye) | 1,806 | 1,829 | 1,681 |
| Ludewa | 1,823 | 1,846 | 1,698 |
| Makambako | 1,777 | 1,801 | 1,653 |
| Makete | 1,816 | 1,839 | 1,691 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 1,783 | 1,806 | 1,658 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **1,866** | **1,889** | **1,741** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 1,866 | 1,889 | 1,741 |
| Kalambo (Matai) | 1,873 | 1,896 | 1,748 |
| Nkasi (Namanyele) | 1,879 | 1,903 | 1,754 |
| **Ruvuma (Songea)** | **1,816** | **1,817** | **1,691** |
| Mbinga | 1,850 | 1,829 | 1,725 |
| Namtumbo | 1,846 | 1,808 | 1,721 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 1,860 | 1,854 | 1,735 |
| Tunduru | 1,875 | 1,782 | 1,750 |
| **Shinyanga** | **1,822** | **1,845** | **1,697** |
| Kahama | 1,835 | 1,859 | 1,710 |
| Kishapu | 1,850 | 1,874 | 1,725 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 1,853 | 1,876 | 1,728 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **1,863** | **1,887** | **1,738** |
| Busega (Nyashimo) | 1,856 | 1,880 | 1,731 |
| Itilima (Lagangabilili) | 1,866 | 1,890 | 1,741 |
| Maswa | 1,855 | 1,878 | 1,730 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 1,862 | 1,885 | 1,737 |
| **Singida** | **1,783** | **1,807** | **1,659** |
| Iramba | 1,796 | 1,819 | 1,671 |
| Manyoni | 1,768 | 1,791 | 1,643 |
| Ikungi | 1,779 | 1,802 | 1,654 |
| Mkalama (Nduguti) | 1,808 | 1,831 | 1,683 |
| **Songwe (Vwawa)** | **1,809** | **1,832** | **1,684** |
| Songwe (Mkwajuni) | 1,816 | 1,839 | 1,691 |
| Ileje | 1,813 | 1,836 | 1,688 |
| Momba (Chitete) | 1,818 | 1,842 | 1,693 |
| Tunduma | 1,813 | 1,837 | 1,688 |
| **Tabora** | **1,847** | **1,870** | **1,722** |
| Igunga | 1,801 | 1,824 | 1,676 |
| Kaliua | 1,866 | 1,889 | 1,741 |
| Ulyankulu | 1,860 | 1,883 | 1,735 |
| Nzega | 1,812 | 1,835 | 1,687 |
| Sikonge | 1,859 | 1,882 | 1,734 |
| Urambo | 1,860 | 1,883 | 1,735 |
| Uyui | 1,848 | 1,871 | 1,723 |
| **Tanga** | **1,654** | **1,693** | **1,987** |
| Handeni | 1,675 | 1,714 | 2,008 |
| Kilindi | 1,690 | 1,729 | 2,023 |
| Korogwe | 1,666 | 1,705 | 1,999 |
| Lushoto | 1,676 | 1,715 | 2,009 |
| Mkinga (Maramba) | 1,661 | 1,700 | 1,994 |
| Muheza | 1,659 | 1,698 | 1,992 |
| Pangani | 1,661 | 1,700 | 1,994 |

**JEDWALI B: BEI ZA JUMLA**

| | Petrol (TZS/Lt) | Diesel (TZS/Lt) | Kerosene (TZS/Lt) |
|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 1,568.35 | 1,591.23 | 1,444.08 |
| TANGA | 1,529.75 | 1,568.28 | 1,862.19 |
| MTWARA | 2,012.68 | 1,606.13 | - |

**JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

| Bandari | | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | Ongezeko la Dola 46.557/Tani | Ongezeko la Dola 50.888/Tani | N/A |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | Ongezeko la Dola 52.062/Tani | Ongezeko la Dola 38.821/Tani | N/A |
| TANGA | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | N/A | N/A | N/A |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | N/A | N/A | N/A |
| MTWARA | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | N/A | N/A | N/A |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | N/A | N/A | N/A |

**JEDWALI D: MWEZI HUSIKA WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA**

| | Aina ya Mafuta | Shehena ya Mafuta Ilipokelewa Mwezi: | Mwezi husika wa Bei za Soko la Dunia zilizotumika mwezi huu: | Mwezi husika wa Bei za Soko la Dunia zilizotumika mwezi uliopita: |
|---|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | Petroli | Juni 2020 | Mei 2020 | Aprili 2020 |
| | Dizeli | Juni 2020 | Mei na Juni 2020 | Aprili 2020 |
| | Mafuta ya Taa | Aprili 2020 | Machi 2020 | Februari 2020 |
| TANGA | Petroli | Aprili 2020 | Machi 2020 | Februari 2020 |
| | Dizeli | Aprili 2020 | Machi 2020 | Februari 2020 |
| | Mafuta ya Taa | Machi 2020 | Februari 2020 | Juni 2019 |
| MTWARA | Petroli | Machi 2020 | Februari 2020 | Januari 2020 |
| | Dizeli | Aprili 2020 | Machi 2020 | Januari 2020 |
| | Mafuta ya Taa | N/A | N/A | N/A |

**Mha. Godfrey H. Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA"**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Umakini unahitajika katika utekelezaji bajeti 2020/21

BAJETI ya serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21, inaanza kutekelezwa rasmi leo, serikali ikitarajiwa kukusanya na kutumia Sh. trilioni 34.88.

Katika bajeti hiyo ambayo ni ya mwisho kwa awamu ya kwanza ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, Sh. trilioni 21.98 zinatarajiwa kutumika kwa matumizi ya kawaida ukiwamo uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, huku Sh. trilioni 12.9 zikitarajiwa kutumika kwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Leo, ikiwa ni siku ya kwanza kabisa ya kuanza kwa utekelezaji wa bajeti hiyo, Nipashe tunaikumbusha serikali umuhimu wa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika bajeti hiyo.

Tunakumbusha vipaumbele hivyo vilivyowekwa katika viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, serikali ikitarajia kujenga viwanda vinavyotumia kwa wingi malighafi zinazopatikana nchini zikiwamo za kilimo, madini na gesi asilia, ili kukuza mnyororo wa thamani.

Katika hili, serikali iimeahidi kutekeleza miradi ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata gesi asilia, uanzishwaji na uendelezaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi na Kongane za Viwanda, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuongeza thamani ya madini na usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu.

Pia, kuweka mkazo katika kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora, pembejeo na zana za kilimo na uvuvi, huduma za ugani na utafiti, uimarishaji wa malambo na majosho, ujenzi wa maghala na upatikanaji wa masoko ya mazao na mifugo ndani na nje ya nchi.

Serikali pia imepanga kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, elimu na ujuzi na huduma za maji safi na salama kupitia utoaji wa elimumsingi bila ada, utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kuboresha huduma ya maji, kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, ununuzi na usambazaji wa dawa pamoja na ujenzi wa hospitali za wilaya na vituo vya afya.

Nipashe tunakumbusha pia uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji kupitia utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu nishati, usafirishaji pamoja na ununuzi na ukarabati wa ndege, meli na vivuko.

Mbali na vipaumbele hivyo, serikali pia inatarajiwa kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kutoa ajira mpya kwa wananchi, hususan vijana waliohitimu vyuo vikuu na maeneo mengine ya kitaaluma.


Vilevile, tunakumbusha ahadi iliyotolewa ya kulipa madeni ya wazabuni, watumishi na mifuko ya hifadhi ya jamii ambako Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebainisha kuwapo kwa deni kubwa na la muda mrefu.

Ni katika mwaka huu wa fedha serikali kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA), itaanza kukusanya mapato yaliyokuwa yanakusanywa na mamlaka za kiuhifadhi likiwamo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro.

Nipashe tunaona kuna haja mamlaka hizi zikakumbukwa na serikali kwa watumishi wake kulipwa mishahara na posho zao kwa wakati ili kuwa na motisha ya kazi sambamba na kutekeleza miradi ya mamlaka hizo kwa wakati ili kulinda hadhi ya utalii nchini.

Pia, Nipashe tunaamini kuwa, bila kuwapo kwa nidhamu katika matumizi, utekelezaji wa bajeti hiyo ya serikali hautafanikiwa, hivyo kuna haja serikali kuendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kuimarisha utawala bora katika usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Vyama vinadhibitije janga wapigakura kutaka rushwa?

Na Mwandishi Wetu

MWEZI Julai barani Afrika ni wakati wa kupambana na rushwa, kila mwaka Julai 11 ni Siku ya Umoja wa Afrika (AU) ya kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa.

Rushwa inatajwa kuwa ni chanzo cha uharibifu, udhalimu, uovu na ndiyo mzizi mkuu wa umaskini barani Afrika na mara nyingi imekuwa ikilelewa na kulindwa na viongozi wengi wa bara hili.

Kwa ujumla mara nyingi wataalamu wa kiuchumi na kisiasa barani Afrika wanaeleza kuwa viongozi wengi wa bara hili ni matunda ya rushwa kwa vile michakato ya uchaguzi inatawaliwa na kuwahonga wanaoteua, kupendekeza na wapigakura. Yote haya yanasababisha uongozi unaolinda maslahi binafsi, wazembe, wabadhirifu, madikteta na mnyororo mzima wa kudumisha na kuendeleza umaskini.

Rushwa ndiyo iliyohujumu na kuteketeza rasilimali za Afrika na kuitumbukiza katika umaskini usiokwisha, ujinga, maradhi na hali duni.

Tanzania inapoelekea kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020, imeweka mikakati ya kuhakikisha kuwa viongozi wa kisiasa hawaendelei kuwa matunda ya rushwa, msimamo huu ukisimamiwa na CCM na serikali.

Wakati huu CCM imetangaza kuwa kupiga vita rushwa ndiyo ajenda kuu na kwamba haitaruhusu viongozi wawe wabunge na madiwani na watendaji wengine wa chama wapatikane kwa njia ya rushwa. Kwa hiyo ili kuunga mkono juhudi za Afrika na serikali kutokomeza rushwa wapigakura wasiwe chanzo cha kutaka rushwa.

Ni ukweli kuwa wapo wapigakura wanaotoa shinikizo kwa kauli na kwa vitendo vyao kuwa wanategemea wafanyiwe jambo maalumu iwe kupewa hongo, nguo, vyakula na chochote ili wapate hamasa ya kujitokeza kwa wingi kumpigia kura mgombea.

Hali hii inashuhudiwa wakati wa kuonyesha nia ya kuteuliwa na chama cha siasa ili kugombea ubunge. Ndiyo kipindi cha kukabaliana na wagombea wanaoonyesha nia wakitakiwa kutoa mlungula.

Wapigakura hutaka kupewa chochote cha ziada na kama hawatapewa pesa huona kama mgombea hana nia ya kupata dhamana anayoitafuta na huachwa kama msindikizaji wa wale `wanaojitoa mhanga' kuwapatia 'soda' au 'chai' wapigakura.

Ni wazi wagombea wana kazi ya ziada kuvuka kiunzi cha kutakiwa kuwahonga wapigakura. Kama nchi ni ukweli usiopingika kuwa kuna janga la mpigakura kudai chake mapema akiamini kuwa mgombea anakwenda kufaidika pekee yake akiwa mbunge na wanaamini kuwa mbunge au kiongozi wa umma ni kuula na kuondokana na umaskini. Lakini pia rushwa ya uchaguzi inayotolewa nje ya kipindi cha kampeni za uchaguzi inayolenga kuwavuta wapigakura imechangia mazoea hayo.

Hapa kuna misaada kama pesa, vifaa na hata wakati mwingine kusaidia familia zenye wahitaji kwa hali na mali kwa malengo ya kutaka uongozi.

Yote haya yanachochea wapigakura kutaka misaada ambayo wakati mwingine hutafsiriwa kama hongo ya uchaguzi nje ya kipindi rasmi cha kufanya kampeni. Kwa kiasi huwafanya wananchi kutaka kupewa kitu kidogo kutokana na kuzoea.

Viongozi wamewazoesha wapigakura kuwapa mlungula kipindi cha kabla ya kutangazwa kampeni za uchaguzi kwa kufanya mambo ya kimaendeleo kwa kutumia raslimali zao au za umma kwenye majimbo yao.

Hii ni rushwa kwani wananchi hupokea baiskeli, pikipiki, mabati, dawa na hata mbegu na mbolea kabla ya uchaguzi ili kuwaandaa kumchagua mhusika kuwa mbunge au diwani wao japo hayo hufanywa mwaka mmoja kabla ya uchaguzi mkuu.

Hayo yote yamefanyika na inachukuliwa kama chai ya uchaguzi, lakini sasa si wakati wa kuendeleza tena jambo hili. Vyama vya siasa vijiulize ni nini kinawasukuma wapigakura kudai rushwa kwa wagombea wao na kwanini wagombea watoe chai?

Jawabu ni kwamba wapigakura huamua kuomba na kuchukua chao mapema kiwe pesa, sukari, kanga, sabuni, chakula au pombe, baada ya kugundua kuwa viongozi wanapochaguliwa huendeleza ubadhirifu na ufisadi.

Kwa hiyo kwa vile viongozi kuanzia sasa wawe wabunge, madiwani na watendaji wengine wa serikali wamepatikana na watapatikana kwa njia halali bila mlungula wananchi hao wataacha mwenendo huo wa kuomba na kutaka rushwa wanapochagua viongozi.

# Waziri azuia 'malipo ya corona' shule binafsi

**Magdalena Haule na Mary Mshami**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, amepiga marufuku wamiliki wa shule binafsi kutaka kutoza malipo ya huduma ambazo hawakuzitoa kwa wanafunzi wakati wa mlipuko wa virusi vya corona.

Amesema kuwa serikali ndiyo iliyotangaza kuzifunga shule zote baada ya mlipuko wa virusi vya corona na yenyewe ndiyo imetangaza kuzifungua, hivyo wamiliki wa shule hizo wanapaswa kutii amri hiyo ya Rais John Magufuli.

Profesa Ndalichako alitoa angalizo jana alipohojiwa na Kituo cha Redio ya Clouds FM baada ya kuwapo kwa malalamiko ya baadhi ya wazazi kuhusu kutopokewa shuleni kutokana na kutokamilisha malipo ya ada na michango mingine.

Waziri huyo pia alikemea kitendo cha baadhi ya wamiliki wa shule binafsi kuwataka wazazi walipie huduma ambazo hazikutolewa na shule zao kwa wanafunzi kipindi cha corona.

"Ni maagizo ya serikali wanafunzi wote warudi, Profesa Ndalichako alisema, "kwa hiyo wanafunzi walioondoka shuleni kwa amri ya serikali na wanatakiwa kurudi shuleni kwa amri ya serikali, tena iliyotangazwa na Rais.

"Tumeweka bayana kwamba ada kwa mwaka, kwa sababu masomo yatakamilika, itabaki palepale, lakini masuala ya usafiri kwa mfano wanafunzi 'wanachajiwa' hela ya usafiri siku ambazo hakuwapo shuleni wakati walikuwapo nyumbani, 'wanachajiwa' kwa misingi ipi?" Profesa Ndalichako alihoji.

"Ugonjwa kwa sasa hivi umepungua. Kwa hiyo, maelekezo ya Rais wanafunzi wote warudi shuleni na sisi tumesimamia wanafunzi wote warudi shuleni. Sasa watakapofika shuleni, kama mlikuwa mnadaiana na hamkufukuzana kabla ya corona, basi mtafukuzana watakapofika shuleni," alisema.

Katika hatua nyingine, Profesa Ndalichako amesema matokeo ya mtihani wa kidato cha sita ulioanza juzi, yatatoka baada ya mwezi mmoja na wiki mbili tangu kukamilika kwake Julai 17 mwaka huu.

"Serikali imejipanga vizuri, wanafunzi watakaomaliza kulingana na ndoto zao, serikali iko tayari kutekeleza ndoto zao," alisema, huku akiwataka wasimamizi kufanya kazi kwa uadilifu kwa kuwa serikali haitamvumilia yeyote atakayekwenda kinyume cha taratibu.

Machi 17 mwaka huu, siku moja baada ya kuripotiwa kwa mgonjwa wa kwanza wa corona nchini, serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ilitangaza kufunga shule na vyuo vyote, ikiwa ni mbinu ya kudhibiti kusambaa kwa virusi hivyo.



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani, Jokate Mwegelo, akizungumza jana wakati akifungua mafunzo ya utalii kwa vijana zaidi ya 52 wa wilaya hiyo. Kushoto ni Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Shogo Sedoyeka na (kulia) ni Ofisa kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Anna Lawuo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC: Vijana Kisarawe badilisheni mitazamo

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, amewataka vijana wa Kisarawe wabadili mitazamo na kujifunza kutafuta fursa zinazopatikana wilayani huko badala ya kusubiri wageni kwenda kuzichukua.

Mwegelo aliyasema hayo jana wilayani huko wakati akifungua mafunzo ya waongoza watalii yanayotolewa kwa siku nne kwa vijana 52 wa Kisarawe.

Mafunzo hayo yanatolewa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Jokate alisema wilaya hiyo ina fursa nyingi za utalii na uhifadhi hivyo lazima vijana wajipambanue kwa kukubali kujifunza na kuzifanyia kazi kwa vitendo fursa zilizomo.

Alisema kwa kufanya hivyo wataweza kujiajiri na kuajiriwa na kuwaletea maendeleo na kukuza pato la serikali.

"Kisarawe kuna fursa nyingi hatupaswi kulalamika kwamba hakuna ajira, ninaamini mkimaliza haya mafunzo hamtakuwa kama mlivyokuja, mtaanza kujiletea maendeleo kupitia rasilimali zilizopo Kisarawe," alisema.

Aidha, Jokate alimshukuru Rais John Magufuli kwa kutoa maelekezo ya barabara kujengwa kwa kiwango cha lami inayotokea Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere kupita wilayani huko hadi hifadhi ya taifa.

"Tunashukuru pia Msitu wa Hifadhi wa Kazimzumbwi na Pugu kupandishwa hadhi, tuna maeneo mengi ya utalii na barabara hii ikimalizika kwa kiwango cha lami, utalii utaongezeka zaidi," alisema.

Alisema mafunzo hayo pia yatatolewa kwa askari wa usalama barabarani, mama lishe na makundi mengine ili kila mmoja atambue wajibu wake katika kuhakikisha eneo lake linapiga hatua kupitia utalii.

Ofisa Utalii Mkuu kutoka TFS, Anna Luwuo, ambaye alimwakilisha Kamishna Uhifadhi, aliwataka vijana hao wazingatie kile watakachofundishwa kwa sababu watalii hupenda watu waaminifu, wanaojua lugha za mawasiliano, maeneo wanakowapeleka watalii na wenye kutabasamu.

Naye, Ofisa Mtendaji Mkuu kutoka Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Shogo Sedoyeka, alimpongeza mkuu wa wilaya hiyo, Jokate kwa kazi anazofanya ikiwa ni pamoja na kuona umuhimu wa kuwapatia vijana mafunzo hayo.

"Tunategemea baada ya mafunzo haya vijana mtajiendeleza kwa kuanzisha bidhaa za utalii, ili uone fursa ni lazima ujuzi ambao ndiyo mnapatiwa," alisema.

## 31 warejesha fomu urais CCM Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANACHAMA 31 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliochukua fomu ya kuonyesha nia ya kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar, wamerudisha fomu zao huku mwanachama mmoja akijiondoa katika kinyang'anyiro hicho.

Uchukuaji fomu ulianza Juni 15 na idadi ya wanachama waliochukua kufikia 32 kati yao watano ni wanawake.

Aliyejitoa mpaka sasa katika kinyang'anyiro hicho ni Hussein Ibrahim Makungu. Watoto watatu wa marais wastaafu ni miongoni mwa watia nia hao wakiwamo mawaziri wa SMZ na wanachama wengine ambao hawana nyadhifa serikalini.

Akizungumza na waandishi wa habari Ofisi Kuu za CCM Kisiwandui baada ya kufunga zoezi hilo jana, Katibu wa Idara ya Oganaizasheni, Galos Nyimbo, alisema watia nia wote wamefuata maelekezo na kutimiza masharti ikiwamo kupata wadhamini 250. "Tunashukuru zoezi limeenda vizuri na watia nia wote wamepata wadhamini 250 kwa mikoa mitatu ya Zanzibar na baadhi yao wamepata zaidi ya wadhamini 250," alisema.

Alisema, watia nia wote walikua na nidhamu na hakuna aliyevunja maelekezo ya chama na zoezi lilikuwa na utulivu wa hali ya juu.

"Nawashukuru wote watia nia wamekuwa na nidhamu ya hali ya juu...utaratibu ulikua mzuri hakuna hata mmoja aliyevunja taratibu kwa mfano tulisema watu wasije na shangwe lolote na wote wamefuata maelekezo hayo," alisema.

Alisema suala la uadilifu na kiwango cha elimu yapo katika mchakato wa vikao vya chama ambavyo vinatarajiwa kuanza leo.

Alisema leo kikao cha sekretarieti kitafanyika na kufuatiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya chama na kikao cha Kamati Maalum cha Halmashauri Kuu ya Taifa, vitafanyika Ofisi Kuu CCM Kiswandui na baada ya hapo vikao vitakavyofuata vitafanyika Makao Makuu ya chama, Dodoma.

"Niwashukuru sana waandishi wa habari tokea mwanzo wa zoezi hili lilipoanza mpo nasi katika kutoa taarifa na leo (jana) tumefikia tamati hongereni sana," alisema Nyimbo.

Wagombea 32 waliochukua fomu ni Mbwana Bakari, Balozi Ali Karume, Mbwana Mwinyi Yahya, Omar Shehe, Muhammed Jafar, Muhammed Hija, Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor, Shamsi Vuai Nahodha, Dk. Hussein Mwinyi, Profesa Makame Mbarawa, Mwatum Mussa Sultan, Haji Rashid Pandu na Dk. Abdul-halim Mohammed Ali, Jecha Salim Jecha na Dk. Khalid Salum Muhamed.

Wengine ni Rashid Ali Juma, Khamis Mussa, Mmanga Mjengo Mjawiri, Hamad Yussuf Masauni, Muhammed Aboud, Bakari Rahid, Ibrahim Makungu, Ayoub Muhammed Mahmoud, Hashim Salum Hashim, Hasna Ataai Maoud na Fatma Kombo Masoud, Pereira Ame Silima, Iddi Hamad Iddi, Shaame Ame Silima, Mussa Aboud Jumbe, Mgeni Hassan Juma na Maudline Castico.

# 'Halmashauri zitumie ramani za wizara'

**Na Munir Shemweta, SONGWE**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezitaka halmashauri nchini kutumia ramani zilizoandaliwa na kutolewa na wizara hiyo kupitia idara yake ya Upimaji na Ramani kwa kuwa ndiyo yenye jukumu la kutafsiri mipaka ya nchi.

Akizungumza wakati akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali mstaafu, Nicodemus Mwengela, ramani mbili za Tanzania pamoja na ile ya Mkoa wa Songwe jana, Dk. Mabula alisema wizara kupitia idara yake hiyo ndiyo yenye mamlaka ya kuandaa na kutoa ramani nchini tofauti na zile zinazotolewa na watu wengine ambazo wakati mwingine zinakuwa na upotoshaji wa mipaka.

Alisema kuwa katika kuepukana na sintofahamu inayoweza kutokea, halmashauri nchini zinapaswa kutumia ramani zinazotolewa na wizara ya ardhi na kuzisambaza katika shule za msingi na sekondari, ili kuepuka aina yoyote ya upotoshaji unaoweza kutokea kwa wanafunzi.

"Ninaziomba halmashauri nchini kutumia ramani zinazotolewa na wizara kupitia idara ya upimaji kwa kuwa inatoa ramani zenye uhakika wa mipaka iliyotafsiriwa na wataalamu tofauti na watu wengine wanaotoa ramani zenye upotoshaji wa mipaka," alisema.

Naibu Waziri huyo ambaye pia alizindua Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Songwe, alisema wizara yake itatoa ramani ya Tanzania kwenye mikoa yote na kubainisha kuwa ramani hizo ndizo zinazotakiwa kutumika kwa kuwa zina vielelezo vinavyokubalika.

Akizungumzia uzinduzi wa ofisi za ardhi katika mikoa, Dk. Mabula alisema uzinduzi wa ofisi hizo ikiwamo ya Mkoa wa Songwe ni jitihada za serikali ya awamu ya tano kusogeza huduma za sekta ya ardhi karibu na wananchi.

Kupitia uzinduzi wa ofisi hizo za ardhi, aliwataka wananchi pamoja na wadau kuzitumia ofisi za ardhi za mikoa kupata huduma za sekta hiyo na kusisitiza kuwa wakifanya hivyo, watakuwa wamekidhi matarajio ya Rais John Magufuli kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi.

Alisema ni muhimu kuwa na hati ya ardhi kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe na kuwaeleza kuwa wanaweza kuitumia katika shughuli za kiuchumi kwa kuchukulia mkopo benki na kutolea mfano wa jinsi hati ya kwanza kutolewa mkoa huo mwaka 1939 Ilivyotumika kuchukulia mkopo na wamiliki wake.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Mwengela, alisema uanzishwaji ofisi za ardhi za mikao utausaidia mkoa wake kutatua migogoro ya ardhi kwa kuwa wananchi wake hawatahitaji tena kwenda umbali mrefu kama ilivyokuwa awali. Kamishna Msaidizi wa Ardhi katika Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Songwe, Suma Mwakasitu, alisema ofisi yake ambayo tayari inazo hati na nyaraka mbalimbali zilizohamishwa kutoka iliyokuwa Ofisi ya Kanda Mkoa wa Mbeya, itaendelea kufanya ziara kwenye wilaya nne inazohudumia kwa lengo la kuwaelimisha wananchi kuhusu huduma inazotoa, ili kuitumia ofisi hiyo.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (katikati) na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali mstaafu, Nicodemus Mwangela, wakiangalia ramani ya mkoa wa Songwe, wakati wa hafla ya uzinduzi ofisi ya ardhi mkoa wa Songwe jana. Kulia ni Kamishna Msaidizi wa Ardhi, Wilson Ruge. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# 54 watiwa mbaroni tuhuma za uhalifu

**Na Alphonce Kabilondo, GEITA**

JESHI la Polisi mkoani Geita limewakamata watuhumiwa 54 kwa makosa mbalimbali, yakiwamo kukutwa na noti bandia za dola za kimarekani.

Aidha, watuhumiwa hao wanadaiwa kukutwa na pombe haramu aina ya gongo, noti bandia fedha za kimarekani dola 2,100 zenye thamani ya shilingi 4,861,500.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Geita, Mtatiro Kitinkwi, akizungumza na wanahabari, alisema kuwa watuhumiwa hao walikamatwa katika operesheni inayoendelea mkoani humo.

Alisema watuhumiwa wawili walikamatwa wakiwa na noti bandia za dola za Marekani 2100 wakitaka kufanya miamala katika benki ya Azania tawi la Katoro wilayani Geita.

Alisema pia waliwakamata waganga wa jadi 10 kwa makosa ya upigaji wa ramli chonganishi pamoja na kukutwa na nyara za serikali.

Aidha, alisema kuwa jeshi hilo limefanikiwa kuwakamata watuhumiwa 15 wakiwa na bangi, huku watuhumiwa 10 walikamatwa wakiwa na gongo lita 1,232 pamoja na mitambo ya kutengenezea pombe hiyo.

Kadhalika Polisi walikamata samani mbalimbali zinazodhaniwa ni za wizi ikiwamo televisheni, sola, mifugo, zana haramu za uvuvi, na kwamba upelelezi utakapokamilika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

# CHAVITA waiomba NEC ushiriki uchaguzi mkuu

**Na Hamisi Nasiri, MTWARA**

CHAMA cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) mkoani Mtwara kimeiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha wenye ulemavu wa kusikia wanapewa fursa na nafasi stahiki ya kushirikishwa moja kwa moja kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2020.

Lengo ni kuhakikisha malengo na mahitaji yao ya msingi yanapewa kipaumbele katika kuchagua na kuchaguliwa.

Aidha, wameiomba NEC kuhakikisha vituo vyote vya kujiandikisha na kupiga kura kunawekwa utaratibu rafiki utakaowasaidia viziwi kushiriki vema katika uchaguzi huo kwa kuweka wakalimani wa lugha ya alama watakaokuwa wanatoa maelekezo kwa kundi hilo wakati wa kupiga kura na michakato mingine katika uchaguzi huo.

Ombi hilo lilitolewa jana wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara na Mratibu wa mradi wa kuimarisha ushiriki wa viziwi katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2020 kutoka CHAVITA mkoa Mtwara, Kasimu Mchindula, alipokuwa akiutambulisha mradi huo unaoendeshwa na CHAVITA mkoa wa Mtwara kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

Mradi huo unawalenga wasimamizi wakuu wa majimbo ya uchauzi na unafadhiliwa na The Foundation For Civil Society.

# Bajaji zakimbiza daladala kwenye stendi ya Zakheim

**Na Fatma Mtutuma, UDOM**

MADEREVA wa daladala wa Mbagala Kiburugwa jijini Dar es Salaam, wameyaondoa magari yao katika stendi ya Zakheim, kutokana na biashara kuwa ngumu.

Wamefanya hivyo kutokana na mabasi kuchelewa kupata abiria, ambao wanapenda kutumia usafiri wa bajaji ambazo zimeongezeka eneo hilo kwa nauli ile ile.

Mmoja wa madereva wa daladala, Said Hamisi, alisema juzi kuwa waliamua kuondoa kabisa magari hayo ili kuzipa nafasi bajaji kutokana na abiria wenyewe kutokuwa wavumilivu.

"Tumeamua kuyaondoa magari yanayokwenda Kiburugwa kutokana na abiria kutokuwa wavumilivu na biashara kuwa ngumu… hivyo ilitulazimu kuyaondoa kwa sababu tulijikuta tunakaa hata saa mbili kusubiria gari lijae," alisema Hamisi.

Aliongeza: "Madereva wa daladala wengi tumehamia katika usafiri wa bajaji tangu usafiri huo ulipopata soko katika stendi hii kuelekea Kiburugwa, binafsi kwa sasa ni dereva wa bajaji."

Mmoja wa madereva wa bajaji, alisema madereva wa bajaji walilipokea kwa furaha kuondolewa kwa daladala, na kwamba biashara kwao imekuwa nzuri kwa kuwa bila bajaji hakuna usafiri mwingine labda pikipiki, ambazo ni gharama kubwa.

HABARI KITAIFA

## Shule ya Bagamoyo yaelemewa wanafunzi

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE ya Msingi Mtambani Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani, yenye wanafunzi 2,400 imeelezea kuelemewa na idadi ya wanafunzi hivyo kuomba msaada wa kuongezewa madarasa 57 kukidhi mahitaji.

Ombi hilo lilitolewa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Timothy Kassiani, wakati akipokea msaada wa kisima cha maji kilichojengwa na shule za Fedha kwa kushirikiana na Asasi ya Time To Help

Alisema shule ina madarasa 16 tu, hivyo inahitaji mengine 57 ili kutosheleza idadi iliyopo.

Alisema idadi hiyo kubwa imesababishwa na ongezeko lisilo la kawaida la uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na wahamiaji.

Naye Ofisa Uhusiano wa taasisi hiyo, Mbwana Kitendo, alisema waliamua kuisaidia shule hiyo kisima chenye thamani ya Sh. milioni 10.

Mbwana alisema wanatarajia kujenga visima 20 katika shule mbalimbali za msingi na sekondari Wilaya ya Bagamoyo. Ofisa Elimu Wilaya ya Bagamoyo (Uchumi), Sophia Kilumbi, aliishukuru taasisi hiyo kwa msaada huo na kuwaomba wasiishie hapo bali waendelee kwenye shule mbalimbali wilaya hiyo.

Mkurugenzi wa Shule za Feza, Ismail Yilmaz, alisema maji ni hitaji la muhimu katika jamii na ndiyo sababu shule zao zimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha watoto wanapata huduma hiyo kuwalinda na magonjwa.

## 'Bodaboda washiriki semina wajue haki'

**Na Halfani Chusi**

OFISA Utawala na Fedha wa Pathway Foundation for the Poor (PFP), amewashauri madereva wa pikipiki nchini, maarufu bodaboda, kujenga utamaduni wa kuhudhuria semina zinazohusu masuala ya usalama barabarani kila mara, ili watambue haki zao na marekebisho ya sheria yanapojitokeza.

Witness Kazoba alitoa rai hiyo jijini Dar es Salaam juzi wakati wa tathmini ya mradi wa uwezeshaji kwa vijana wa bodaboda, akisema bodaboda wengi ni wagumu katika kuhudhuria mafunzo ya elimu inayohusu masuala ya usalama barabarani.

"Sisi kwa kupitia ufadhili wa Serikali ya Uholanzi, tumeandaa mradi unaojihusisha na utoaji wa elimu kwa bodaboda, ili waweze kutambua haki zao, lakini unakuta mwitikio ni mdogo sana, hali inayokatisha tamaa wakati elimu hii ni kwa ajili yao wenyewe," alisema.

Kazoba ambaye ni Msimamizi wa Mradi wa Kuinua Bodaboda, aliongeza: "Lengo la elimu inayotolewa kupitia mradi huu ni kuwajengea bodaboda uwezo katika uongozi, ujasiri, kutambua haki zao, elimu ya usalama barabarani kushiriki vyema katika vyombo vya uamuzi na shughuli za maendeleo ya jamii."

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini katika mradi huo, Karim Kindole, alisema mradi huo licha ya kufanikiwa kufikisha elimu kwa zaidi ya bodaboda 1,845, bado unakabiliwa na vikwazo kadhaa.

# Mkandarasi apewa siku 7

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (sekta ya ujenzi), Mhandisi Elius Mwakalinga, amempa siku saba mkandarasi anayejenga barabara ya Rudewa-Kilosa, kuja na mpango mkakati wa kuhakikisha barabara hiyo inakamilika kwa wakati.

Alitoa agizo hilo baada ya Rais John Magufuli kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 24.

Juzi, Rais Magufuli akiwa katika hafla ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara hiyo, licha ya kutoridhishwa na kasi ya ujenzi huo, alitoa muda wa mwezi mmoja kwa mkandarasi huyo kufanya mabadiliko chanya endapo anataka kuendelea na ujenzi wa mradi huo.

**Hakikisheni mnajenga imani kwa serikali yenu ili iwaamini, hivyo muweze kupata miradi mingi ya ujenzi hapa nchini na hivyo kukuza uchumi wa nchi na ajira kwa wazalendo.**

Akizungumza katika kikao cha dharura kati ya Katibu Mkuu Mwakalinga, Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) na mkandarasi wa Umoja-Kilosa JV, Mhandisi Mwakalinga alimtaka mkandarasi huyo kuhakikisha barabara hiyo inakamilika kwa haraka na kwa ubora uliokusudiwa ili kuiwezesha serikali kuwa na imani na makandarasi wazawa.

"Hakikisheni mnajenga imani kwa serikali yenu ili iwaamini, hivyo muweze kupata miradi mingi ya ujenzi hapa nchini na hivyo kukuza uchumi wa nchi na ajira kwa wazalendo," alisema.

Alisema nia ya serikali ni kuwawezesha makandarasi wazawa kuwa na uwezo na mtaji na hivyo kujenga miradi mingi ya ujenzi ili fedha nyingi inayolipwa kwa makandarasi kubaki nchini na kuhuisha uchumi na kukuza ajira za Watanzania.

"Kuungana, uaminifu, uzalendo na kuchapakazi kwa bidii, kutaiwezesha serikali kutoa miradi mingi ya ujenzi kwa makandarasi wazawa na hivyo kuwajengea uwezo wa kimtaji, utaalamu na uzoefu na kuongeza ajira kwa Watanzania," alisema Mwakalinga.

Barabara ya Rudewa-Kilosa, ni sehemu ya barabara ya Dumila-Kilosa-Mikumi yenye urefu wa Km 142, inayotarajiwa kukamilika Januari mwakani

Itakapokamilika, barabara hiyo itaunganisha mikoa ya Tanga, Morogoro na Iringa bila kupita mbuga ya wanyama ya Mikumi na hivyo kupunguza ajali katika mbuga hiyo.



Wafanyabiashara wadogo wenye sare wakisaka wateja katika basi, stendi kuu ya mabasi Msamvu Mjini Morogoro mwishoni mwa wiki. Walisema sare zinawafanya watambuliwe na uongozi wa stendi hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# EWURA: Hakuna tatizo la petroli

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imewahakikishia wateja wa mafuta ya petroli kuwa kuna lita 92,435,539 kwenye maghala zitakazotosheleza matumizi kwa siku 25.

Pia kuna lita 147,398,593 za dizeli zitakazotosheleza matumizi kwa siku 29 na taarifa za kuwapo kwa uhaba wa mafuta hayo mamlaka inazifuatilia kupitia wakaguzi wake wa mikoa na wilaya.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, alisema hakuna tatizo la mafuta nchini.

Pia alisema maghala hayo ya mafuta yana lita 98,077,624 za petroli na lita 147,404,384 za dizeli kwa ajili ya soko la nje. Chibulunje aliwataka wananchi kununua mafuta kwa bei elekezi iliyotolewa na serikali.

Alisema tayari kampuni 22 zina hifadhi ya mafuta ya petroli katika Bandari ya Dar es Salaam na kampuni 27 zina hifadhi ya mafuta ya dizeli.

"Katika maeneo yaliyotambulika kuwa na uhaba wa mafuta mamlaka ililekeza vituo vya mafuta kununua petroli na dizeli kutoka kampuni mbalimbali ikiwamo Moil, Total, Oryx, Star Oil na Olympic Petroleum," alisema.

Alisema hadi Juni 27, EWURA iliwezesha mafuta kufikishwa au kupakiwa katika maghala kuelekea maeneo yenye uhaba ambayo ni Chato, Chunya, Geita, Ifakara, Ngara, Sirari, Kasulu, Tabora, Nkasi na Vwawa.

"Juni 29, mafuta mengine yanatarajiwa kwa ajili ya kuelekea Geita, Biharamulo, Kibondo, Ilula, Iramba, Igunga, Kondoa, Kibaigwa, Mpwapwa, Kibondo, Kongwa, Mbande, Mvumi, Mlali, Manyoni na Kyela," alisema.

Chibulunje alisema shehena ya petroli yenye tani 39,772 inategemewa kuwasili nchini Julai Mosi.

# Mkataba wa TMDA kuboresha utoaji huduma kwa wateja

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA), imezindua mkataba wa huduma kwa wateja, toleo la nne la mwaka 2020, wenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma.

Kaimu Mkurugenzi wa TMDA, Adam Fimbo, alitangaza kuanza kwa mkataba huo katika hafla ya uzinduzi huo iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema mkataba huo unalenga kupunguza muda wa kusajili dawa zinazotoka nje ya nchi kutoka siku 240 hadi siku 180 za kazi. Alisema kuwa pia wamepunguza muda wa usajili wa dawa zinazotengenezwa ndani ya nchi kutoka siku 120 hadi kufika siku 60, sawa na nusu ya muda wa awali.

**Taasisi zote zinapaswa kuandaa mkataba kama wa TMDA au kitengo maalum cha huduma kwa wateja ili wanaopatiwa huduma wawasilishe kero na malalamiko yao.**

Vilevile, alisema muda wa usajili wa maeneo ya biashara za bidhaa zinazodhibitiwa na TMDA umepunguzwa kutoka siku 10 hadi nane.

"Pamoja na kupunguza siku za kutathmini na kusajili dawa, tumeweka pia utaratibu rahisi wa kusajili dawa ambazo zimekwisha sajiliwa kupitia jumuiya zetu za kikanda kama EAC na SADC pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO)," alisema.

Fimbo alisema hawajapunguza sana siku za kufanya uchunguzi kwenye maabara zao kutoka siku 21 hadi 20 za kazi kwa sababu taratibu za uchunguzi zinahitaji muda wa kutosha kuandaa sampuli, njia za uchunguzi, kupima vifaa na kemikali kabla ya uchunguzi.

Awali, alisema sababu za kuandaa mkataba huo ni kubadilika kwa majukumu ya mamlaka kutoka TFDA na kuwa TMDA, uwekezaji mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha huduma, msukumo katika kukuza sekta ya viwanda na hivyo sera na taratibu zimepitiwa.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Abel Makubi, akizundua mkataba huo kwa Niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Profesa Mabula Mchembe, alizikumbusha taasisi zote za umma kuandaa mikataba ya kurahisisha utoaji huduma nchini.

Alisema taasisi zote zinapaswa kuandaa mkataba kama wa TMDA au kitengo maalum cha huduma kwa wateja ili wanaopatiwa huduma wawasilishe kero na malalamiko yao badala ya kwenda ngazi za juu.



Mratibu wa mradi wa kuimarisha ushiriki wa viziwi katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2020 kutoka Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Mkoa wa Mtwara, Kasimu Mchindula (wa pili kulia), akiutambulisha mradi huo katika ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, alipotembelea jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Benki yashauri w'biashara kutumia bima

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imewashauri wafanyabiashara kutumia huduma mbalimbali za bima zinazotolewa na benki hiyo, kulinda biashara zao pamoja na mali nyingine ili kujikinga na majanga anuai yanayoweza kurudisha nyuma biashara.

Kauli hiyo imetolewa na Meneja Mwandamizi wa Bima Benki ya NMB, Martine Massawe, jijini Arusha, alipokuwa akiwatembelea wafanyabiashara mbalimbali pamoja na kukabidhi nyaraka za bima kwa baadhi walioijiunga na huduma za bima.

Alisema bima kwa mfanyabiashara ni muhimu sana kwani inamfanya aweze kufanya biashara yake kwa kujiamini, kwani hata kama itapatwa na majanga kama ya uhalifu, moto au maafa mengine mteja atasaidiwa na biashara kurejea kama awali.

Aliongeza kuwa kwa kutambua umuhimu wa huduma za bima kwa wateja wake, sasa ina uwezo wa kumkopesha mteja ili afanikiwe kukata bima kisha mteja kurejesha taratibu, huku biashara yake ikiwa salama muda wote.

"Sasa hivi mteja mwenye sifa tunaweza kumkopesha fedha kisha akakata huduma ya bima aitakayo kulingana na mahitaji yake, na mkopo huo ataulipa taratibu huku tayari biashara yake ikiwa salama, tunatambua usalama wa biashara ya mteja wetu ni jambo la msingi," alisema Massawe.

Alishauri Watanzania kujenga utamaduni wa kukata bima mbalimbali ili kujikinga na majanga ambayo yamekuwa yakiwarudisha nyuma kiuchumi yanapotokea.

Benki ya NMB imeanza kutoa huduma za bima katika matawi yake yote nchini baada ya kuzindua huduma ya bima kupitia benki (Bancassurance) uliofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

Huduma za bima zitakazopatikana katika matawi ya Benki ya NMB ni pamoja na zile za kampuni za Sanlam Life, UAP, Shirika la Bima la Taifa (National Insurance Corporation - NIC), Jubilee, Shirika la Bima la Zanzibar na Reliance.

## Wanafunzi walia ugumu wa usafiri

**Na Mary Mshami,** UDOM

WANAFUNZI wakazi wa Banana, Ilala jijini Dar es Salaam wamelalamikia ugumu wa usafiri kuwa ni changamoto kwao hasa kipindi hiki baada ya shule kufunguliwa Jumatatu.

Shule zote nchini zilifunguliwa na serikali baada ya kupungua maambukizi ya homa ya mapafu (Covid-19) inayosababishwa na virusi vya corona.

Wakizungumza na Nipashe katika kituo cha Banana, juzi walisema ni changamoto kubwa sana kwao kwa kuwa hata wakipakizwa wanne katika daladala bado wengi wanakosa usafiri.

"Mimi nimekuja hapa kuanzia saa kumi na moja, gari sipati yakija yamejaa, mimi naona tutafutiwe suluhisho lingine hii maana haisaidii na hata hiyo kuruhusiwa wanne hata hatutoshi bado," alisema mmoja wa mwanafunzi hao.

Baadhi ya abiria waliunga mkono kuwa usafiri ni mgumu siyo kwa wanafunzi tu, bali hata watu wazima tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa abiria kutosimama maarufu 'level seat'.

## Taasisi yasaidia shule Ilala vifaa vya corona

**Na Sabato Kasika**

JAMII imetakiwa kuendelea kuwatunza watoto baada ya shule kufunguliwa kwa kuwaelimisha wajiepushe na mambo yanayoweza kusababisha maambukizi ya corona.

Akikabidhi msaada wa vifaa mbalimbali vya kujikinga na corona kwa wakuu wa shule za msingi, sekondari na wa Mpango Maalum wa Elimu (MEMKWA), Kaimu Meneja Mradi wa Shirika la SOS, Jacqueline Haule, alisema wameguswa na kulazimika kutoa msaada huo ili wanafunzi shuleni wawe kwenye mazingira salama.

Msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 65 unahusisha barakoa, ndoo za maji, matangi na vitakasa mkono, na utatolewa kwa wanafunzi wa shule za sekondari nne na msingi 11 za Kata ya Chanika na Zingiziwa, wilayani Ilala jijini Dar es Salaam.

"Kupitia miradi yetu mbalimbali ukiwamo 'tuimbe na tucheze' imetekelezwa na kuonyesha mafanikio makubwa katika shule tunazozisaidia kwani watoto wamekuwa na ari ya kupenda kwenda shule na utoro umepungua," alisema.

Naye, Mratibu wa Kituo cha Walimu Chanika na Zingiziwa, Nancy Peter, alisema ukanda huo una shule nyingi, na kwamba vikao mbalimbali vimefanyika ngazi ya kata hadi mkoa ili kuwalinda watoto na walimu wasipate maambukizi ya Covid-19.

Malawi yavunja rekodi ya Kenya

Ukurasa 13





Ukurasa 12

## Kada CCM ataka mgombea binafsi, adai kuegemea chama kumepitwa

siasa

JUMATANO JULAI 1, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

KUTUMBULIWA VIGOGO

# Viongozi wataka vyote wametafakari njia zao?

**Na Mary Geofrey**

JULAI 2016, baada ya Rais John Magufuli, kukabidhiwa uenyekiti wa CCM, alibainisha changamoto na mambo ambayo anataka yabadilike ndani ya chama.

Mosi aliainisha kupiga vita rushwa ndani ya chama, kuondoa usaliti, unafiki, kung'angania madaraka, kujilimbikizia vyeo na maslahi.

Akiwahutubia wajumbe 2,893 wa Mkutano Mkuu wa CCM uliohudhuriwa na mabalozi na wawakilishi wa vyama vya siasa, anatilia mkazo suala la kumaliza changamoto ya wanachama kung'ang'ania vyeo.

Aidha, Mwenyekiti anatumia nafasi hiyo kutuma salamu kwa Wana- CCM, walizoea kununua nafasi za uongozi kwenye uchaguzi na kuwaambia mambo hayo yanaelekea ukingoni.

Anakumbusha kuwa serikali yake haitalivumilia hilo na halitajitokeza na kwamba wakati akigombea urais alishuhudia wajumbe wa CCM wa mkoa wa Iringa wakiwa wamenunuliwa.

"Vyeo hivi tumevitengeneza ili kutengeneza migogoro wakati wa uchaguzi, najua nimegusa watu humu unakuta Waziri anavyeo vingi, tunazuia wana CCM kupata madaraka kwa sababu ya mtu mmoja kuwa na vyeo vingi,"

Wakati Rais Magufuli anayaeleza hayo ni wazi kuwa wajumbe wa mkutano ule walishangilia na kuyaacha maneno hayo pale bila kuziangatia kuwa ni jambo walilotakiwa kulifanyia kazi na kulitekeleza kwa vitendo.

Kwanini liliachwa pale kwenye mkutano, inadhihirika pale Rais Magufuli anapowatengua viongozi kwa sababu za kushindwa kutekeleza mambo wanayotumwa na chama na serikali.





Viongozi wa zamani Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mrisho Gambo na Mkuu wa Wilaya ya Arusha Gabriel Daqarro , uteuzi wao ulitenguliwa hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO.**

Hivi karibuni aliwatumbua viongozi wa mkoa wa Arusha akiwamo Mkuu wa Mkoa Mrisho Gambo, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo, Dk. Maulid Madeni.

Wakati akiwaapisha wateule wapya kuchukua nafasi zao waliondolewa anaawaambia viongozi hao Idd Kimanta, Mkuu wa Mkoa , Kenan Kihongosi Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Jiji John Pima, kuwa sababu ya kutengua uteuzi ni uroho wa madaraka na tamaa na kulumbana.

Anakumbusha kuwa CCM na serikali yake inatekeleza msimamo uliotolewa mwaka 2016 kuwa hakuna kulea waroho wa maradaka na wanaotaka kujilimbikizia vyeo.

Rais Magufuli anawaonya viongozi wakiwamo wateule wake wanaosaka ubunge wakati huu wa kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba kuwa ni bora waridhike na nafasi walizonazo.

Anawataka watendaji na viongozi waliopo madarakani wajifunze kuridhika na nafasi walizonazo.

"Nitashangaa kama IGP -Mkuu wa Jeshi la Polisi atakwenda kugombea ubunge Bunda, ategemee nitamteua kuwa waziri.

"Ningemtaka awe waziri si ningemteua tu kwenye nafasi za wabunge halafu nikamteua waziri, lakini nilimteua yeye akawe IGP wa Tanzania nzima.

"Sasa ukitoka hapa ukagombee Bunda na wakati mwingine useme nitakuteua kuwa waziri kwanza huna uhakika kama utashinda kura za maoni na inawezekana ukashinda lakini bado nikafuta na hii itatokana na siku hiyo nimeamkaje," anasisitiza Rais Magufuli.

"Hamuwezi mkawa na kila kitu lakini demokrasia ipo huru kama una uhakika ukienda kule utashinda tu, basi nenda kwa speed (kasi) kubwa," anasisitiza.

**HATUA ANAZOCHUKUA**

Rais Magufuli akiwa katika hafla hiyo, hakuacha kueleza sababu za kutengua uteuzi wa watendaji hao watatu wa mkoa wa Arusha, akisema kila mmoja kuwa bosi kwa mwenzake na kufanya mambo binafsi badala ya yale aliyowaagiza.

Anaeleza kusikitishwa na wateule hao kutokuwajibika na kuendekeza tamaa na hisia binafsi .

Anasema ni matumiani yake aliowateuwa watakwenda kutimiza wajibu wao na kushirikiana na watakaowakuta ili kuisimamia miradi mingi iliyopelekwa kwenye jiji hilo.

Ni jambo jemba kukumbushana kuhusu haya ambayo Rais Magufuli anayayatekeleza kwa vitendo kabla ya kwenda kuacha nafasi yako ya uongozi na kuwania nafasi ambayo huna uhakika kama utashinda.

Ni wakati pia wa kutambua kuwa zama za viongozi kuwa miungu watu, kuamua nini kifanyike na nini kisifanyike kwa matakwa binafsi na siyo kwa mujibu wa kanuni na taratibu za nchi, zimeisha.

Ifahamike kuwa kama ambavyo chama hicho, kilivyokwisha weka msimamo wake kuhusu mtu mmoja kushika nafasi moja, unatekelezwa kwa vitendo.

Suala hili ni wazi kuwa linaaminisha kuwa uongozi ni dhamana, kiongozi ana wajibu wa kuwatumikia anaowaongoza na siyo wananchi kumtumikia kiongozi.

Ni jambo jema lenye manufaa kwa CCM na lenye maslahi kwa taifa lakini ni kilio kwa watu ambao wanataka uongozi kwa ajili ya maslahi binafsi na siyo kwa manufaa ya umma.

Ni wazi kuwa suala hili litasaidia kuongeza uwajibikaji kwa watendaji na kuridhika na nafasi walizonazo kwa sababu kama bado kungeendelea kuwa na fursa ya mtu mmoja kushika nafasi zaidi ya moja ni wazi kuwa kunaondoa maana na uongozi.


Katibu Mkuu Mstaafu wa CCM, Abdulrahman Kinana, alikuwa kiongozi aliyetembea nchi nzima kukagua ilani ya chama hicho ya mwaka 2010/15 pamoja na kuthubutu kukikosoa chama chake na serikali hadharani, hatua iliyozaa matokeo ya kukemea viongozi kujilimbikizia mali.

Muhimu serikali na chama kuendelea kulikemea na kulishikia bango suala hili na zaidi kila mwanachama wa chama hicho, kutambua wajibu wa chama ili kuondoa uozo uliokuwa ukifanywa na watendaji miaka ya nyuma kwa sababu za uroho wa madara.

Mwisho

### KUELEKEA UCHAGUZI MKUU...

# Kada CCM ataka mgombea binafsi, adai kuegemea chama sasa basi



Thomas Ngawaiya akichangia hoja bungeni enzi hizo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

KATIBA ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza mfumo na utaratibu wa kupata viongozi wa kisiasa-rais, wabunge na madiwani.

Kwa mujibu wa ibara ya 39(1)(c) mgombea yeyote wa nafasi hizo ni lazima awe amependekezwa na chama cha siasa. Kwa hiyo hakuna mgombea nje ya utaratibu huo.

Aidha, ibara ya 67(1)(b) ya katiba hiyo inasema mbunge ni lazima apendekezwe na chama chake na hakuna mgombea anayepatikana tofauti na maelekezo hayo.

Halikadhalika, Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2010 inazungumzia uteuzi wa wagombea na kuelekeza kuwa ni lazima watokane na vyama vya siasa vilivyosajiliwa na kutambulika kisheria.

Hata hivyo, mmoja wa makada wa CCM, inaona kuwa utaratibu huo unatakiwa kuangaliwa upya, akieleza kuwa unasababisha baadhi ya wanachama wenye uwezo wa kuongoza kukosa nafasi hizo hasa wale ambao hawapendwi na viongozi wakuu wa vyama vyao wanaosimamia uteuzi na kupendekeza wagombea.

Ni maoni ya Thomas Ngawaiya, anayeshauri kuwapo kwa mabadiliko, ambayo yatawezesha Tanzania kuwa na mgombea binafsi ili kuondoa mfumo huo.

Mwanasiasa huyo anasema, si jambo la ajabu kutoa ushauri huyo, kwa vile unalenga kusaidia kila Mtanzania mwenye sifa za kuongoza aweze kupata nafasi hiyo, kupitia chama au nje ya mfumo huo.

Anasema, hiyo ndiyo njia pekee ya kuwezesha Watanzania kushika nafasi mbalimbali za uongozi, vinginevyo wengi wataendelea kukwama kupata uongozi kwa sababu ya mfumo wa kupitia kwenye vyama vya siasa.

Mwanasiasa huyo, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (Cegodeta), anafafanua kuhusu hoja yake katika mahojiano na gazeti hili, jijini Dar es Salaam.

> Anasema, hiyo ndiyo njia pekee ya kuwezesha Watanzania kushika nafasi mbalimbali za uongozi, vinginevyo wengi wataendelea kukwama kupata uongozi kwa sababu ya mfumo wa kupitia kwenye vyama vya siasa.

***SWALI: Imekuaje leo umeibuika na hoja hii ya mgombea binafsi?***

**JIBU:** Hii hoja siyo ya leo wala juzi. Kwenye miaka fulani iliyopita, nikiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji John Tendwa, tulizungumzia sana mgombea binafsi na alielekea kuona kwamba ni jambo la maana linalowezekana, lakini muda wake uliisha na mimi muda wangu wa ubunge wakati ule ulimalizika, basi hakuna aliyeendeleza tena, lakini bado ninasema kwamba, mazungumzo yangu yalikuwa yamezungumzia sana kwamba, hawa watu wanaotaka wagombea binafsi tuwapo ruhusu, uandaliwe muswada na kupelekwa bungeni na kupitishwa, haitaleta madhara yoyote.

Leo hii ninakumbushia tena kwamba, kuna hatari gani kuruhusu mgombea binafsi? Turuhusu mgombea binafsi naye anaweza kuleta changasmoto zake, kwa sababu kama yupo wa kushinda atashinda tu.

***SWALI: Msingi wa hoja yake ya kutaka mgombea binafsi ni upi?***

**JIBU:** Ukiangalia ndani vyama vya siasa, utabaini kwamba kuna changamoto nyingi ambazo wakati mwingine zinaweza kuwa ni kikwazo kwa baadhi ya watu wanaotaka uongozi. Hivyo njia pekee ni kuruhusu utaratibu wa mgombea binafsi.

Kwanza kabisa silengi chama bali ninazungumzia changamoto zilizomo ndani ya vyama vya siasa.

***SWALI: Kuna changamoto gani kwenye vyama vya siasa?***

**JIBU:** Kwenye baadhi ya vyama vya siasa kuna viongozi ni kama miungu watu hawataki kuguswa, hivyo wako tayari kumfanyia mtu mizengwe asiweze kugombea nafasi katika chama na pia kukiwakilisha chama dhidi ya vyama vingine. Hivyo njia pekee ni kuwapo kwa mgombea binafsi, ili kama mwanachama atawekewa mizengwe katika chama chake, basi awe mgombea huru. Hivyo ninaiomba serikali iangalie upya uwezekano wa kuwa na mgombea wa kujitegemea wasiofungamana na vyama.

***SWALI: Kuna manufaa gani zaidi ya kuwa na mgombea huru kuliko kupitia vyama?***

**JIBU:** Mifumo yote miwili ina umuhimu wake ila tatizo ni mizengwe ambayo imekuwa ikifanywa na baadhi ya viongozi wa vyama na kusababisha hata wagombea ambao wananchi wanawataka wanaachwa, kwa sababu tu wenye madaraka katika vyama hawawataki. Hivyo mfumo wa mgombea huru au binafsi utaondoa changamoto hizo na unaweza kusaidia kupata viongozi wazuri. Ndiyo maana ninasema, wasinyimwe hiyo nafasi kwa sababu ya mfumo wa kupitia katika vyama. Nirudie kuishauri serikali iangalie uwezekano wa kuruhusu mgombea binafsi, kwani Tanzania inajengwa na watu wote hata wasiokuwa wanachama wa vyama vya siasa.

***SWALI: Unadhani kwamba utaratibu wa mgombea binafsi ukiruhusiwa nchini, wapo watu ambao wanaweza kuutumia?***

**JIBU:** Watu wapo na ndiyo ambao wamekuwa wakilalamikia mchakato wa kupata wagombea katika vyama vyao. Kwa hiyo kama ambavyo Katiba anatambua haki ya mtu kuchagua au kuchaguliwa, ninaamini hata katika hili suala la mgombea binafsi ni haki, kwa sababu lengo ni kuchaguliwa. Kama kupitia chama mgombea atawekewa mizengwe, basi awe mgombea huru kwa sababu ni haki yake ya kikatiba kuchaguliwa.

Mtu akiwa mwanachama au hayupo katika chama, anayo haki inayotokana na uraia wake kupiga kura na ya kupigiwa kura.

***SWALI: Suala la mgombea binafsi halikuanza leo, unadhani ni kwa nini halijafanyiwa kazi?***

**JIBU:** Ni kweli halikuanza leo, ndiyo maana nilikuambia kuwa nililianza mwanzoni mwa mwaka 2000 nikiwa mbunge, lengo ni kupanua demokrasia yetu. Ninaamini kwamba kinachokwamisha ni uamuzi tu, ndiyo maana ninaiomba serikali iangalie uwezekano wa kuruhusu mgombea binafsi. Ikumbukwe kuwa suala hili ni miongoni mwa mambo muhimu, kwani hata katika Rasimu ya Katiba Mpya ilizingatia jambo hili ingawa Bunge Maalum la Katiba halikuona umuhimu wake.

***SWALI: Kuna jambo ambalo mara nyingi huwa huliweki wazi, nalo ni kugombea ubunge. Je, utakuwa miongoni mwa wana CCM wanatakaochukua fomu kuwania nafasi hiyo?***

**JIBU:** Mimi kugombea ubunge nasema hapana, kwa sababu, kwanza umri wangu, nawaachia vijana , halafu kazi nimefanya nyingi sana za utumishi, ni vyema kukaa nielekeza wenzangu, tushirikiane kuchagua na kuangalia ambao wanafaa tuwapigie debe. Tuwape maelekezo, kuliko mimi tena kwenda kugombea. Nimeshakuwa Mwenyekiti wa Jumuiya wa Wazazi ya CCM Mkoa wa Kilimanjaro, mbunge Moshi Vijijini. Nimeshafanya kazi kwenye Kurugenzi ya Makumbusho ya Taifa kwa miaka mitano, kwa kweli utumishi huu pia na umri wangu, napaswa kuheshimu umri wangu, naona nina mawazo mengi ya kushauri hao watakaoingia kwenye utawala kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu.

# Malawi yavunja rekodi ya Kenya

## •Yapata Rais anayependa kuimba hata akiwa bafuni

**Na Mashaka Mgeta**

KENYA iliweka historia kwa mahakama nchini humo kutengua matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2017, lakini sasa Malawi imeipiku kwa kuwa nchi ya kwanza Afrika kufuta matokeo ya uchaguzi wa urais na kuandaa duru ya pili na upinzani kuibuka na ushindi.

Mwaka 2017, upinzani Kenya ulichukua hatua hiyo iliyofanyika Malawi, kupinga matokeo ya uchaguzi wa urais yaliyotenguliwa na mahakama, lakini kinara wa upinzani nchini humo, Raila Odinga wa ODM alisusia duru ya pili

na kusababisha 'ushindi wa kishindo' kwa Rais Uhuru Kenyatta wa chama cha Jubilee.

Hali kama hiyo ya kususia uchaguzi, ilijitokeza katika uchaguzi wa 2015 visiwani Zanzibar ambapo aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi visiwani humo, Jecha Salum Jecha aliufuta uchaguzi na kuitisha uchaguzi wa marudio ambao chama kikuu cha upinzani visiwani humo, Civic United Front (CUF) kiliususia.

Wachambuzi wa kisiasa wanasema matokeo ya uchaguzi kutokana na kutowajibika kwa tume limeendelea kuwa tatizo sugu barani Afrika na kuwa katika nchi nyingi.

Mahakama na tume za uchaguzi ni vyombo vinavyoongozwa na wateuliwa wa marais waliopo madarakani na hivyo kuwa kishawishi cha kuelemea upande wa waliowateuwa.

Gambia inatajwa kuwa miongoni mwa nchi chache kwa kuwa na tume yenye uadilifu, ikitolewa mfano kuwa mwaka 2017, ilimtangaza kiongozi wa upinzani Adama Barrow kuwa mshindi halali dhidi ya rais aliyekuwa madarakani kwa muda mrefu Yahya Jammeh.

Tukio kama hilo la mabadiliko ya kidemokrasia katika kanda ya kusini mwa Afrika, liliwahi pia kujitokeza Zambia ambapo rais wa kwanza Kenneth Kaunda, alikubali kushindwa na mpinzani wake Frederick Chiluba.

**NI HISTORIA MALAWI**

Katika uchaguzi mkuu uliofanyika Juni 23, mwaka huu, aliyekuwa mgombea urais kupitia chama cha Malawi Congress Party (MCP), Lazarus Chakwera, alishinda kwa kupata asilimia 58.57 dhidi ya rais aliyekuwa madarakani, Dk.Peter Mutharika aliyepata kura 1,751,377 na nafasi ya tatu kuchukuliwa na Peter Dominico

Kuwani aliyeambulia kura 32,456 huku waliojitokeza kupiga kura wakitajwa kuwa ni asilimia 64.81.

Kiongozi huyo amekuwa akijihusisha na kamati ya masuala ya umma yenye misingi ya kidini na mashirika ya kutetea haki za kiraia, akiwa kama mtetezi wa masuala ya uongozi bora.

Rais huyo mpya wa Malawi anayezungumza Kiingezera cha lafudhi ya Kimarekani anasema anapenda kusoma na muziki wa kiasili, wa kigeni na nyimbo za



Rais Lazarus Chakwera. **PICHA: BBC**

> Gambia inatajwa kuwa miongoni mwa nchi chache kwa kuwa na tume yenye uadilifu, ikitolewa mfano kuwa mwaka 2017, ilimtangaza kiongozi wa upinzani Adama Barrow kuwa mshindi halali dhidi ya rais aliyekuwa madarakani kwa muda mrefu Yahya Jammeh.

Injili.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, anapenda kuimba sana hata akiwa peke yake bafuni akioga.

Kwa ujumla uchaguzi huo wa duru la pili ulifanyika baada ya mahakama nchini humo kuyafuta matokeo ya uchaguzi wa awali yaliyompa ushindi Mutharika.

Katika uchaguzi huo, Mutharika alitangazwa kupata ushindi mwembamba wa kura 159,000 - sawa na asilimia 38.6 ya kura zilizopigwa huku Chakwera akifuatia kwa nafasi ya pili akiwa na asilimia 35.4.

Chakwera na mgombea aliyekuwa katika nafasi ya tatu walipinga matokeo hayo kwa madai kwamba uchaguzi huo haukuwa huru na haki.

Miongoni mwa hoja zao ni kwamba nakala za kuhesabu kura zilifutwa na kuongezewa idadi ya kura kwa kutumia wino wa kusahihisha makosa.

Kupingwa kwa matokeo hayo kulizua maandamano na ghasia kati ya wafuasi wa upinzani na polisi nchini humo.

Ingawa maelfu ya raia wa Malawi walishangilia kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa awali, Mutharika akautaja uamuzi huo kama "mabadiliko yanayoadhimisha mwanzo wa mwisho wa demokrasia nchini humo."

Licha ya kutenguliwa kwa matokeo ya awali, aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi nchini humo, Jane Ansah alijiuzulu kufuatia miezi kadhaa ya shinikizo la waandamanaji waliomkosoa kwa jinsi alivyosimamia uchaguzi huo.

Ushindi wa Chakwera dhidi ya Mutharika licha ya kuungwa mkono na wapinzani wengine, unakirejesha madarakani chama kilichoasisiwa na Dk Banda cha Malawi Congress MCP kwa mara ya kwanza, miaka 26 baada ya kuondoshwa madarakani.

Baada ya matokeo ya awali kuonyesha kwamba kimeshindwa, kilichokuwa chama tawala cha Democratic Progressive Party (DPP) kilitoa wito wa kurudiwa kwa uchaguzi huo kwa madai ya kukumbwa na udanganyifu na vitisho.

DPP ikaitaka tume ya uchaguzi nchini humo kutupilia mbali matokeo hayo na kutaka kufanyika kwa uchaguzi wa tatu.

Katibu wa chama hicho Francis Mphepo, anasema, "tungependa kuangazia matukio kadhaa ambayo huenda yakataja dosari uaminifu na uadilifu wa matokeo ya ya uchaguzi wa urais."

Chama hicho kiliorodhesha vituo ambavyo kilidai wasimamizi wake walitolewa nje na kusema zaidi ya kura milioni 1.5 zilichakachuliwa.

"Hakuna shaka yoyote kwamba vitendo vya udanganyifu vitaathiri matokeo kwa namna moja au nyengine,"Mphepo anakaririwa na vyombo vya habari akisema.

**BAIBAI IKULU**

Siku nne baada ya kufanyika kwa uchaguzi huo, Mutharika hakuwa na namna nyingine zaidi ya kuanza kuizoea hali ya kuondoka ikulu, pale aliposema ingawa hakubaliani na matokeo lakini Malawi na Wamalawi walipaswa kusonga mbele.

Chakwera ameapishwa kuwa rais mpya wa Malawi kupitia hafla iliyofanyika jijini Lilongwe.

Mwandishi wa BBC Kusini mwa Afrika, Andrew Harding, anasema si jambo la kawaida kwa mahakama za nchi za Afrika kufuta matokeo ya urais, ingawa suala hilo linawavutia watu wengi pale mahakama inapoingilia kati na kubadilisha matokeo katika eneo ambalo wizi wa kura ni suala la nyeti.

Baada ya matokeo rasmi kutangazwa Chakwera anautaja ushindi huo kuwa ni ishara thabiti ya demokrasia na haki, huku akiweka wazi namna roho yake ilivyojawa na furaha.

**MAANA YA USHINDI**

Matokeo ya uchaguzi huo yametafsiriwa kwa namna tofauti na wachambuzi wa masuala ya siasa, wengi wao wakielezea sababu kuwa ni hatua ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na mahakama nchini humo, kujitenga na ushawishi wa ikulu au watawala.

Baada ya kufutwa kwa matokeo ya awali, Mutharika alikata rufani katika mahakama ya rufani kupinga uamuzi huo, lakini akashindwa.

**MUTHARIKA AFUNGUKA**

Kama ilivyokuwa kwa wapinzani katika matokeo ya uchaguzi wa awali, Mutharika naye akautaja uchaguzi wa duru la pili kwamba ni mbaya zaidi uliowahi kushuhudiwa nchini humo."Ni uchaguzi ambao haki haikutendeka."

Akizungumza baada ya kupiga kura kusini mwa Malawi, Mutharika alidai na kukaririwa na Shirika la Habari la Reuters, kwamba kulikuwa na ghasia katika maeneo ya upinzani.

"Inasikitisha. Katibu Mkuu wetu amepigwa, wanaosababisha ghasia hawana la kufanya," alinukuliwa akisema na kisha kuhoji, "ni vipi sasa kwamba uchaguzi huu utakuwa wa haki na huru?"

**KUUNGANISHA TAIFA**

Vyombo kadhaa vya habari vimekariri vyanzo tofauti vukielezea kwamba pamoja na mambo mengine, Rais Chakwera anakabiliwa na changamoto ya kuwaunganisha Wamalawi kufuatia mgawanyiko uliojitokeza, na kumaliza ghasia zilizoshuhudiwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Hali hiyo inawiana pia na kudhibiti vitendo vya ufisadi, kupunguza umaskini na ukosefu wa ajira, mambo ambayo yalikuwa ni miongoni mwa masuala ya msingi katika uchaguzi huo.

Shirika la habari la AFP, limesema kuwa Rais huyo anapenda kuimba sana hata akiwa peke yake bafuni akioga.

MAHOJIANO MAALUM

# Zitto Kabwe: Kwa safu hii ACT tunavyoiona, tumejipanga hivi

- Ajigamba ana wanachama wa kutosha
- Ziara yake Kusini adai 'kuna shida ufuta'

**Na Enock Charles**

JANA katika sehemu ya kwanza ya mahojiano haya maalum na Nipashe, Zitto Kabwe, Kiongozi Mkuu wa chama cha ACT-Wazalendo na Mbunge wa Kigoma Mjini, alianika misimamo yake 'adimu' kuhusu hatua yake inayofuata katika siasa. Ufuatao ni mwendelezo wa baadhi ya dodoso zilizojificha na ameamua kuziweka bayana:

---

***SWALI: Mara kadhaa ulisimama bungeni na kuzungumzia mustakabali wa zao la ufuta. Kuna mafanikio katika hoja yako hiyo?***

**ZITTO:** Tumekuwa tukifuatilia... eeh kuhusiana na zao la ufuta tangu tumeanza ziara mikoa ya kusini, hasa Lindi, kwa kuzungumza na wakulima na wafanyabiashara, yaani wachuuzi wanaonunua ufuta kwa wakulima kuhusiana bei na ambazo wanategemea kuuza kwenye soko la kimataifa.

Mwaka jana ufuta uliuzwa kwa zaidi ya 2,160 (kwa kilo) na mwaka huu umeshuka bei mpaka Sh. 1,600, jambo ambalo tunaona litaleta madhara makubwa kwa wakulima kwa sababu hata gharama ambazo zilitumika kwa ajili ya kulima, kukusanya na kupeleka ghalani kwa kilo moja zitazidi hiyo Sh. 1,600.

Sasa, muhimu tuna mambo mawili -- kwanza ni jambo la haraka kwamba serikali ni lazima ihakikishe kwamba soko la ufuta lisiharibike kama ambavyo soko la ufuta lilivyoharibika kwa sababu itakuwa ni kuwatia umaskini wananchi wa mikoa inayolima ufuta ambayo ndiyo hiyohiyo mikoa inayolima korosho.

La pili, sisi kama chama cha ACT-Wazalendo, tuna jawabu kuhusiana na changamoto za bei za mazao kwani toka mwaka 2015 tumekuwa tukihamasisha na kushauri kwamba iundwe mfumo wa hifadhi ya jamii kwa wakulima ambao unaweza ukawa na kitu kinachoitwa fao la bei ili bei inaposhuka sana chini ya gharama za uzalishaji wakulima wanaweza wakarejeshewa zile gharama za uzalishaji kutokana na hilo fao la bei.

Lakini, bahati mbaya serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) haijasikia kabisa mawazo haya kutoka ACT-Wazalendo. Kwa hiyo, sisi tunachowahamasisha wananchi ni kwamba tutakapounda serikali na siyo lazima iwe serikali kuu, hata serikali za mamlaka za serikali za mitaa



ama halmashauri, tutahakikisha tunaunda mfumo wa hifadhi ya jamii kwa wakulima, ili kuwa na mazingira ambayo bei zikiporomoka kuona kuwa wakulima wanaweza wakafidiwa wa bei ili wasianguke kwenye dimbwi la umaskini.

***SWALI: Mpaka sasa, ACT-Wazalendo mna wanachama wangapi?***

**ZITTO:** Mpaka sasa rekodi zetu zinaonyesha kuwa tumetoa kadi kwa zaidi ya watu milioni moja na uhakiki bado unaendelea kufanywa na chama makao makuu ili kupata uhalisia ule wa wanachama hai kwa sababu unaweza kuwa umewapa watu kadi na kuna walioenda vyama vingine.

Na kuna watu wengine ni wanachama na wamejiorodhesha, lakini hawajapatiwa kadi. Kwa hiyo, namba hiyo inaweza ikawa kubwa zaidi ya hapo, lakini kwa ujumla kwa sasa kwa mujibu wa rekodi zetu tuna wanachama zaidi ya milioni moja kutokana na kadi ambazo tumezitoa.

***SWALI: Kwa hali ilivyo kisiasa nchini, mna matarajio ya kufanya vizuri katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu?***

**ZITTO**: Matarajio yetu katika uchaguzi ni kwanza tujitahidi kufanya ushirikiano na vyama vingine vya upinzani kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunaweka nguvu kwenye kuhami demokrasia yetu kwa sababu umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Kwa hiyo, hilo ndiyo la kwanza. La pili, tunatarajia kushiriki kikamilifu kwenye uchaguzi kuhakikisha kwamba tunakuwa na wabunge wengi, mabaraza mengi ya miji na halmashauri ambazo tutaziongoza na ushindi wa Rais wa Zanzibar na vilevile ushindi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ama kwa kushirikiana na vyama vingine ama kwa sisi wenyewe.

Bado tunaendelea na mazungumzo ya ushirikiano wa vyama na muda utakapokamilika, tutaujulisha umma ni hatua gani ambayo tumefikia na mazungumzo hayo yanatupa mwelekeo gani.

***SWALI: Takriban wanachama 30 wa CCM wamejitokeza kuomba ridhaa ya chama kuwania urais wa Zanzibar. Ni yupi kati ya hao walioijitokeza mnamwona atakuwa tishio kwenye ikiwa atapitishwa na chama hicho tawala?***

**ZITTO:** Hakuna mgombea tunayemwogopa kati ya hao wote. Kikubwa, wamalizane wenyewe. Tunawasubiri walete mgombea wao tumchakaze.





# Wanakijiji waondokana na adha ya maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKAZI wa Kijiji cha Mayeto, Wilaya ya Dodoma, wameondokana na adha ya maji baada ya kuanza kuchimbwa kwa kisima cha maji.

Wananchi hao awali walilazimika kutembea umbali wa kilomita nne kufuata huduma ya maji huku wanawake wakihatarisha ndoa zao kwa kuamka usiku wa manane kusaka maji.

Wakizungumza jana wakati wa uzinduzi wa sehemu kitakapochimbwa kisima cha maji cha kijiji hicho, mbele ya Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu,Kazi, Ajira na Vijana ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, wananchi hao waliishukuru serikali na Mbunge kwa kuwaletea kisima hicho.

Mkazi wa eneo hilo,Kenneth Ndagwa, alisema wana furaha kupata maji kwani mke wake alikuwa akiamka asubuhi kutafuta maji hali ambayo ilikuwa ikihatarisha ndoa yake.

"Furaha tuliyonayo moyoni mwetu wananchi wa Kitongoji cha Mayeto na Mtaa wa Mayeto, kwa kweli nina furaha sana moyoni mwangu na hata machozi yanataka kutoka kwa sababu ni muda mrefu sana tumekuwa tukipata shida sana juu ya maji, lakini Mungu ametenda na Mungu amefanya, tunapenda sana kukushukuru Mbunge wetu kwa hichi ambacho umefanyia wana mtaa wa Mayeto," alisema.

**Wakati wa uzinduzi wa gari la kusafirishia wapendwa wao pindi wanapofariki walimpa kero ya maji pamoja na kukosekana kwa shule ya msingi ambapo aliahidi kuzitatua.**

Aliongeza: "Maana yake kwamba hata Taifa la Israel walipokuwa katika nchi ya utumwa, waliteseka sana wakiwa chini ya mfalme Farao, lakini Mungu anamtuma Mussa, anakwenda kuliokoa Taifa la Israel wanapata ukombozi.

"Lakini nawe umetumwa kuja kutuletea ukombozi wananchi wa Mtaa wa Mayeto, maana yake kwamba watu walikuwa wanatoka Mayeto kwenda Makulu ni kilomita nne ilikuwa ni shida sana, watu walikuwa wanateseka sana, kuoga ilikuwa ni shida.

"Mungu akubariki sana,wakati mwingine hata mke wangu anaposafiri kwenda kuchota maji anasafiri kwa saa nne nakuwa na wasiwasi sana lakini leo(jana) umetuwezesha kwamba ndoa yangu itakuwa na uaminifu kwa sababu ya maji yamekuwa karibu, ubarikiwe sana.

"Tunakufananisha na Mussa, umekuja kutukomboa katika shida hii ya maji, tutaendelea kukuombea na endapo utagombea kura za hapa utazipata mpaka uje ufe ,kura za hapa hutakuja kukosa hata moja," alisema Ndagwa.

Naye, Janeth Ndagwa alisema walikuwa na kero ya muda mrefu ya maji hivyo wanashukuru kupata kisima hicho hivyo wanamwomba Mbunge huyo kuukamilisha mradi huo kwa wakati ili waache kutembea umbali mrefu.

Neema Faru, mkazi wa eneo hilo, alisema walikuwa wanapata shida ya maji na walikuwa wakiamka saa 10 alfajiri kwenda kutafuta maji, huku wakiwaacha waume zao kitandani.

"Tulikuwa tunapata shida sana ya maji, tulikuwa tunaamka saa 10 usiku tulikuwa tunavisima hapo korongoni, yaani ukichelewa tu unakuta wenzako wamemaliza maji unakaa mpaka saa nane hujapata maji.

"Ukirudi lazima tu utagombana na mume wako,mara nyingine na uzee wangu huu nilikuwa napanda baiskeli hadi Makulu, nabeba dumu tatu kama huna baiskeli unaenda kwa mguu unavuka mlima huu unabeba dumu moja ukiondoka saa 11 alfajiri unarudi saa nne asubuhi tunamshukuru sana Mavunde,tunamuombea kwa mungu,"alisema.

Mavunde aliwashukuru wananchi hao kwa uvumilivu mkubwa waliounesha licha ya kukosa maji kwa muda mrefu pamoja na kutembea umbali mrefu kutafuta maji.

Alisema wakati wa uzinduzi wa gari la kusafirishia wapendwa wao pindi wanapofariki walimpa kero ya maji pamoja na kukosekana kwa shule ya msingi ambapo aliahidi kuzitatua.

"Hii ndio Serikali ya awamu ya tano ya kutatua matatizo ya msingi, niliwaambia maneno yangu yanaishi, nilitafuta mradi huu miaka minne iliyopita na nilikuwa ninauhakika maji yatapatikana ninafuraha tunaanza kuchimba kisima sasa na shule tulianza kujenga.

Alisema ataendelea kushirikiana na wakazi hao kwa kuhakikisha huduma zote muhimu wanazipata.

"Lakini ninachokisema kwenu katika muda wote bado tutaendelea kushirikiana kutatua chagamoto za Hombolo Makulu.

"Mngeweza kuhisi kwamba maneno yalikuwa ni ya kufurahisha, kati ya jambo ambalo ninaliogopa ni kusema uongo katika jambo ambalo linatoa matumaini,niliahidi nilikuwa ninauhakika

## Siku ya Dawa za Kulevya yaadhimishwa kwa usafi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kupambana na Dawa za Kulevya nchini (YOVARIBE), imeadhimisha Siku ya Dawa ya Kulevya Duniani kwa kufanya usafi katika eneo la kituo cha Polisi cha Kati jijini Dodoma, na kutoa elimu kwa vijana.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Yeovariki Dunia, alisema wameamua kufanya usafi, katika kituo cha polisi ili kudhihirisha kuwa vijana hao hivi sasa wamepona na hawatumii tena dawa za kulevya.

Alisema lengo lao ni kuona vijana wote wanaotumia dawa za kulevya, wanakuwa funzo kwa wengine ambao wanajiingiza katika utumiaji.

"Tumeazimisha siku ya madawa ya kulevya duniani kwa kufanya usafi sehemu mbalimbali, ili kuwaonyesha kwamba vijana wanaotumia dawa wamepona," alisema Dunia.

Alifafanua kuwa lengo lao ni kuona kila kijana ambaye anatumia dawa za kulevya anakuwa mwalimu kwa wengine ambao wanatumia dawa hizo.

Alisema wanaiomba serikali kuendelea kutoa msaada kwa taasisi, ambazo zinajihusisha na kupambana na matumizi ya dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema kwa upande wa Jiji la Dodoma, vijana zaidi ya 100 walikuwa wanatumia dawa za kulevya wamepona na wanaendelea na shughuli mbalimbali katika taasisi hiyo.

Pia alisema wanaendelea kutoa tiba kwa wengine ambao wanajihusisha na dawa za kulevya, ili waache na kuwa mfano kwa wengine ambao wanaendelea kutumia dawa hizo.



Wakazi wa Kitongoji cha Bwawani, Kijiji cha Ngwandi, wilayani Chamwino, Mkoa wa Dodoma, wakitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari kuhusu jengo la shule (pichani), lililojengwa kwa nguvu kazi, ambalo limeshindwa kupauliwa zaidi ya miaka minne. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## W'biashara wa soko wamwomba RC

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA zaidi ya 100 wa matunda katika soko la Sabasaba jijini hapa, wamemwomba Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Bilinith Mahenge, kuangalia suala la ushushaji wa mizigo ili kuwapunguzia gharama kutokana na sasa mizigo yote ikitakiwa kushukia soko jipya la Job Ndugai.

Walisema hayo jana wakati wa mkutano wao ambao pia ulihudhuriwa na Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Michael Ngoi, alisema wamekuwa wakiingia gharama kubwa kusafirisha mikungu ya ndizi.

"Kulitolewa tangazo kuwa magari yote makubwa na madogo yashushie mizigo Nanenane kwenye sojo jipya, jambo hili linatugharimu sana tunawaza baada ya miezi mitatu mitaji itakuwa imekata kabisa," alisema.

Alisema kabla ya kutolewa kwa agizo hilo, mizigo ilikuwa ikishushiwa viwanja vya barafu na gharama ya kusafirisha mkungu moja mpaka sokoni ilikuwa ni Sh. 700 lakini sasa gharama ya kusafirisha mkungu moja wa ndizi ni Sh. 2,600.

"Mzigo ukishukia soko jipya ukitaka kusafirisha kwenda soko la

Sabasaba gharama ni kubwa, kushusha kila mkungu ni Sh. 200, kubeba Sh. 200, kupakia Sh. 1,500, ukifika sokoni kushusha na kupeleka ndani ni Sh. 400 na hiyo ni gharama ya mkungu moja tu wa ndizi.

Mfanyabiashara mwingine, Matanza Matanza, alisema waliwahi kupeleka malalamiko kwa mkuu wa mkoa, lakini mpaka sasa hajajibiwa.

Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema suala la kushusha mizigo soko la Ndugai lilitolewa na Mkuu wa mkoa, Dk. Mahenge.

"Pale mfanyabiashara anapokuwa na hoja anasikilizwa, mkuu wa mkoa wakati anasema hayo alikuwa na nia njema tu, kuna wafanyabiashara soko jipya kwa hiyo mizigo ikishushwa pale wafanyabiashara wa pale wawe wananuanua mizigo soko la jumla na kupanga kwenye vizimba vyao," alisema.

Alisema hoja zao amezichukua na zitafikishwa mamlaka husika. "Hoja zenu nitazifikisha mamlaka husika na mtapatiwa majibu," alisema





# Urejeshaji mikopo waitesa Rungwe

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe, inakabiliwa na urejeshaji hafifu wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Imeelezwa kuwa hali ambayo inasababisha vikundi vingine kushindwa kunufaika.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Omary Mungi, wakati wa kukabidhi mkopo wa Sh. milioni 151 kwa vikundi 27 vya wajasiriamali katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Alisema kati ya Sh. milioni 332 ambazo halmashauri hiyo ilikuwa imekopesha mpaka Machi mwaka huu, ni Sh. milioni 82.4 pekee ndizo zimesharejeshwa na vikundi hivyo ambavyo ni sawa na asilimia 25 ambayo ni nusu ya lengo.

Alisema kwa mujibu wa utaratibu wa mikopo hiyo, ilitakiwa mpaka sasa asilimia 50 iwe imerejeshwa kwa ajili ya kukopesha vikundi vingine, lakini kutokana na tatizo hilo la urejeshaji ndio maana hata fedha walizokopesha katika robo ya mwisho ni kidogo.

**Serikali haipendi kuwaletea polisi kwa ajili ya kuja kuwakamata, lakini ikitokea ndio hiyo huwa tunalazimika kufanya hivyo, Mkurugenzi wetu huwa hapendi habisa kufikia hatua hiyo hasa kwenu wanawake wenzake.**

"Asilimia 75 ya fedha ambazo tulivikopesha vikundi ukiacha hizi za leo (juzi) bado hazijarejeshwa, sasa mikopo hii inatolewa bila riba ya aina yoyote, lakini bado wananchi wanakuwa wazito kurejesha, hii inatakiwa irejeshwe ili tukopeshe vikundi vingine," alisema Mungi.

Aliwataka wanaokopeshwa fedha hizo kuwa waaminifu ili wawe na sifa za kukopesheka wakati mwingine, na kwamba wanatakiwa wazitumie kwa malengo yaliyokusudiwa badala ya kubadili matumizi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Laurance Kibona, alisema fedha ambazo vikundi hivyo vinakopeshwa zinatokana na mapato ya ndani ukiwamo ushuru wanaotozwa kwenye biashara zao.

Alisema kutokana na hali hiyo, wananchi wanatakiwa kuacha kukwepa kulipa ushuru na kodi ambazo wanatozwa na serikali kwa maelezo kuwa sehemu ya malipo hayo zinarudi kwao kwa njia ya mikopo isiyokuwa na riba.

Dk. Kibona alivitaka vikundi vinavyokopeshwa fedha hizo kuhakikisha vinairejesha kwa wakati ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani kwa maelezo kuwa hilo sio lengo la serikali.

"Serikali haipendi kuwaletea polisi kwa ajili ya kuja kuwakamata, lakini ikitokea ndio hiyo huwa tunalazimika kufanya hivyo, Mkurugenzi wetu huwa hapendi habisa kufikia hatua hiyo hasa kwenu wanawake wenzake," alisema Dk. Kibona.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Mnkondo Bendera, alisema elimu inatakiwa zaidi kwa vikundi vya wanufaika ili wajue umuhimu wa kurejesha mikopo hiyo kwa wakati.

Alisema kuna uwezekano wananchi hao wakashindwa kurejesha mikopo hiyo kwa sababu hawana elimu ya kutosha ya ujasiriamali, hivyo wakikopeshwa wanafanyia shughuli zingine.

"Mtu ambaye ana elimu kama ana pikipiki mbili ataongeza ya tatu, lakini kwa yule ambaye hana elimu ya ujasiriamali, akipata mkopo huo anaweza akaongeza mke tofauti na lengo la serikali kwa hiyo toeni elimu," alisema Bendera.

Alivitaka vikundi vyote ambavyo vimeshanufaika na mikopo hiyo kurejesha kwa wakati ili vikopesheke zaidi na fedha hizo zinufaishe vikundi vingine.



Baadhi ya wananchi wakipita sehemu ya lango kuu la stendi ya mabasi ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi Tarafani, mkoani Mbeya jana, ambayo inafanyiwa ukarabati licha ya kuwa na mwezi mmoja tangu ilipokamilika na kuanza kutumika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Hifadhi yakabidhiwa chanzo cha maji

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

SERIKALI wilayani Makete Mkoa wa Njombe imeukabidhi uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Kitulo chanzo cha maji cha Igofi katika Kata ya Kinyika ili kudhibiti uharibifu wa mazingira unaofanywa na baadhi ya wananchi wanaofanya shughuli za kibinadamu.

Aidha, imeagiza wanaolima na kuchungia mifugo katika maeneo yanayozunguka chanzo hicho waondolewe kwa nguvu na kuwataka maofisa wa hifadhi hiyo kusimamia uondoaji wa miti ambayo siyo rafiki kwenye vyanzo vya maji.

Maagizo hayo yalitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Makete, Veronica Kessy, alipokuwa anazindua mradi wa ufugaji wa nyuki wa kikundi cha watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (HIV) cha Kijiji cha Kinyika ambacho kilipatiwa mizinga 300 ya nyuki na Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) kupitia Hifadhi ya Taifa ya Kityulo.

Alisema mbali na kuondoa miti ambayo siyo rafiki kwenye vyanzo vya maji, pia wanatakiwa wasimamie upandaji wa miti rafiki ili chanzo hicho kiendelee kudumu na kuwanufaisha wananchi wa kijiji cha Kinyika na maeneo mengine.

"Mmenialika kuja kuzindua mradi huu, lakini mimi nina mamlaka kisheria kutoa maagizo, kuanzia leo nataka hiki chanzo kisimamiwe na Hifadhi ya Kitulo... na hii kwa sababu ni taasisi ya serikali basi hiki chanzo kitatumika kwa ajili ya maslahi ya taifa zima," alisema Kessy.

Aliupongeza uongozi wa hifadhi hiyo kupitia kitengo cha ujirani mwema kwa kuamua kukisaidia kikundi hicho cha wananchi wanaoishi na VVU kwa maelezo kuwa mizinga hiyo itakisaidia kuwaongezea kipato bila kuathiri mazingira.

Kaimu Mkuu wa Hifadhi ya Kitulo, Suzan Tesha, alisema mizinga waliyotoa pamoja na vifaa vya kulinia asali vina thamani ya Sh. milioni 16.5.

# Wanachama watamba kuvaa sare za CCM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, kimesema kwa sasa wanachama wake wana uwezo wa kutembea katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo wakiwa wamevaa sare za chama tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Hayo yalisemwa juzi na Mwenyekiti wa CCM Mbeya Mjini, Afrey Nsomba, wakati alipokuwa anazindua tawi la wakereketwa wa chama hicho katika eneo la Soko la Kimataifa la Mwanjelwa, ambapo alisema awali watu walikuwa wanaogopa kuvaa sare hizo wakihofia kushambuliwa.

Alisema kwa sasa wanachama hawaogopi na baadhi ya waliokuwa wanafanya matukio ya kuwashambulia wanaovaa sare za CCM wamejiunga na chama hicho baada ya kuelewa sera zake vizuri tofauti na walivyokuwa wanaaminishwa awali na vyama vya upinzani.

"Hili eneo ilikuwa ni vigumu sana mtu kutembea ukiwa umevaa sare za CCM, sasa hivi watu mmekielewa chama na mmeamua kuanzisha mpaka tawi hili... sasa hivi sera za chama chetu zimeeleweka vizuri na kazi zinazofanywa na viongozi wenu mnaziona na kuamini."

Aliwataka wanachama wa chama hicho katika tawi hilo kuendelea kueneza sera za chama hicho kwa wananchi ambao sio wanachama wa CCM ili na wao wajiunge.

Nsomba alisema serikali imefanya mambo mengi ya maendeleo katika Jiji hilo licha ya kwamba lilikuwa linaongozwa na upinzani ikiwamo kwenye sekta ya afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Alisema muda ukifika chama hicho kitawaeleza wananchi miradi ambayo serikali imetekeleza ili waifahamu na wajue manufaa yake kwao.

Naye Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mbeya Mjini, Philimon Mng'ong'o, alisema Rais John Magufuli ni miongoni mwa marais bora barani Afrika, na kwamba ndio maana wananchi wanakiamini chama hicho.

Alisema chama hicho kinawataka wananchi kuendelea kukiamini chama hicho na kuhakikisha wanashirikiana kuhakikisha Jimbo la Mbeya Mjini linakombolewa kutoka upinzani.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara katika soko hilo, Adam Mwakatumbula, alisema wafanyabiashara wa soko hilo wanaielewa serikali, na ndio maana waliamua kuanzisha tawi hilo ambalo awali ilikuwa ni vigumu kuanzishwa kwenye eneo hilo.





# Katibu wa Mufti atoa ufafanuzi madrasa, vyuo Quran

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU wa Mufti Zanzibar, Khalid Mfaume Ali (pichani chini), amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijaruhusu kufungua madrasa za vyuo vya Quran pamoja na madrasa za watu wazima.

Hayo aliyasema huko ofisini kwake Mazizini Mjini Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tamko la kusimamisha madarasa ya watu wazima pamoja na masomo ya madrasa kwa watoto.

Alisema kufuatia tamko la kuruhusiwa shughuli za kijamii ikiwamo harusi na mambo mengine, watu wengi walifahamu kuwa kila jambo lililokatazwa kutokana na maradhi ya corona tayari yamesharuhusiwa.

Alisema zilizoruhusiwa ni shule na sio madrasa, hivyo ziendelee kusubiri mpaka maelekezo mengine yatakapotolewa.

Alieleza kuwa kufunguliwa kwa shule haina maana kuwa ndio muhimu zaidi kuliko madrasa, unatafutwa utaratibu maalum ili kuweka hali ya usalama.

Aliwaomba masheha na walimu wote wa madrasa waendelee kusubiri na kutoa ushirikiano na anaamini wananchi wote watafuata kikamilifu maelekezo yaliyotolewa.



# Wizara yahimiza ushirikiano sekta elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema ushirikiano mzuri baina ya wizara yake na wadau mbalimbali wa maendeleo utasaidia kuendelea kupiga hatua katika sekta hiyo.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhiwa ndoo za kuoshea mikono zilizotolewa na Jumuiya ya Al Ansaar kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kiislamu ya Muzdalifa kwa ajili ya shule mbalimbali zenye upungufu wa vifaa hivyo ili kuwakinga watoto na corona.

Alisema ili kuwalinda wanafunzi ni vizuri kushirikiana na wadau walio tayari kutoa misaada ili kuhakikisha wanasoma wakiwa salama kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

**Ndoo 400 za kunawia mikono zimekabidhiwa Wizara ya Elimu kutoka jumuiya hiyo kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kiislamu ya Muzdalifa.**

Waziri Pembe aliipongeza jumuiya hiyo kwa msaada huo na kuwaambia fadhila zake hazitoishia duniani bali hata ahera.

Aliishukuru Jumuiya ya Muzdalifa kwa juhudi zao kubwa wanazoendelea za kutoa misaada mbalimbali katika sekta ya elimu nchini ambayo inasaidia kupiga hatua katika maendeleo ya sekta hiyo.

Naye Mkuu wa Miradi wa Jumuiya ya Al Ansaar ust Haji Juma, alisema wameamua kutoa msaada huo kutokana na changamoto hasa katika kipindi hiki cha kufunguliwa shule kukiwa bado na tishio la corona.

Aliiomba Wizara ya Elimu kuendelea kupokea misaada yao ili kusaidia kupunguza changamoto ndogo na kupiga hatua za kielimu nchini.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kiislamu, Muzdalifa Mwalimu Abdalla Hadhar, alisema jumuiya yao inafanya shughuli mbalimbali za maendeleo nchini hasa sekta ya afya na elimu ili kuwa na jamii yenye mwamko mzuri na maendeleo.

Mwanafunzi Latifa Mohamed Ali kutoka Shule ya Kiembe Samaki kwa niaba ya wanafunzi wenzake, alipongeza Wizara ya Elimu na jumuiya hizo za kimaendeleo kwa kuhakikisha wanafanya bidii kuwasaidia wanafunzi ili waweze kusoma katika mazingira salama hasa kutokana na janga lililoikumba dunia la maradhi ya Covid-19.

Ndoo 400 za kunawia mikono zimekabidhiwa Wizara ya Elimu kutoka jumuiya hiyo kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kiislamu ya Muzdalifa, ambazo zitagawiwa katika shule mbalimbali za Unguja zenye upungufu wa vifaa hivyo.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kulia), akipokea msaada wa ndoo za kunawia mikono kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kiislamu ya Muzdalifa, Abdallah Hadhar kwa kishirikiana na Jumuiya ya Al Ansari, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wazanzibari wakumbushwa kudumisha mila

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZANZIBARI wametakiwa kulinda, kuzienzi na kutangaza mila na desturi zinazowatambulisha kwenye mataifa mengine ili kuwa endelevu na vizazi vijavyo.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Sherehe za Kijadi za Mwaka Kogwa, Mwita Masemo Makungu, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, Makunduchi katika Kijiji cha Koba, Wilaya ya Kusini Unguja.

Alisema miongoni mwa mila za Wazanzibari ni sherehe za Mwaka Kogwa ambazo hufanyika Makunduchi kila mwaka ambazo kwa sasa zinatambulika kuwa ni sherehe za kitaifa na huhudhuriwa na wageni wa ndani na nje ya nchi.

Alieleza kuwa sherehe hizo ni miongoni mwa mila na utamaduni ulioletwa na watu waliotoka Bara la Asia na kufikia katika kijiji hicho cha Makunduchi na mwanzo walikipa jina la 'Kae kuu' lenye maana ya sehemu inayoishi watu.

**Sherehe za Mwaka Kogwa ni miongoni mwa mambo wanayojivunia kutokana na kusherehekewa na watu wa mataifa mbalimbali na kuwa chanzo cha mapato kwa taifa.**

Naye Katibu wa kamati hiyo, Ali Khatibu Ali, alisema sherehe za Mwaka Kogwa ni miongoni mwa mambo wanayojivunia kutokana na kusherehekewa na watu wa mataifa mbalimbali na kuwa chanzo cha mapato kwa taifa.

Aliwataka wananchi wa Kijiji cha Makunduchi kuwa wakarimu kwa wageni watakaohudhuria sherehe hizo kwa kuwapikia chakula cha asili na kuwatembeza sehemu za kihistoria za kijiji chao.

Kwa upande wake Mjumbe wa Kamati ya Mwaka Kogwa, Haji Ramadhan, aliwataka vijana kuhudhuria kwa wingi maadhimisho hayo ambayo ni ya asili hasa kwa wale wenye asili ya Makunduchi.

Aliwataka watakaohudhuria sherehe hizo zinazotarajiwa kufanyika Julai 17 kuwa na tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NO.17/2020**
**(Kutokana na shauri la maombi Na.93/2017 Mahakama Kuu ya Tanzania Mbeya,Asilia shauri la Ardhi Na.7/2016 Baraza la Ardhi Na Nyumba wilaya ya Rungwe)**

MARIA RAPHAEL.......................................MWOMBAJI
DHIDI YA
1. HURUMA JOSEPH (Msimamizi wa mirathi ya marehemu Joseph James Mwalukoba)
2. MOSES K.MAGANGA.............................MJIBU MAOMBI
3. HTT INFRANCO......................................MJIBU MAOMBI
4. VODACOM..............................................MJIBU MAOMBI

Kwa:MOSES K.MAGANGA
POPOTE ULIPO
KUITWA SHAURINI MJIBU MAOMBI NA.2

Unaamriwa na Mahakama hii uhudhurie hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya tarehe 02/07/2020 siku ya Alhamisi saa 3.00 asubuhi,ambapo shauri limepangwa kutajwa.

ELEWA KWAMBA:Ukikosa kufika siku hiyo shauri litapangwa kusikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 01 mwezi Juni,2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

157940

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI**
**(MCA)/62**
**Mahakama ya mwanzo ya: KATORO**
Wilaya ya: GEITA.
Madai Namba 45/2020
Mdai: EMANUEL $ MALEKAMA@MAGESA
Mdaiwa: CHAUSIKU $ SYLIVESTER
WA KATORO.

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/ wameleta madai yake/ yao kwamba.

**MADAI YA KUACHANA NA MKE**
**(TALAKA)**

Kwa hiyo unaitajiwa/ mnaitajiwa kuhudhuria kwa binafsi mahakama. Mahakama hii siku ya IJUMAA tarehe 03/07/2020 asubuhi kujibu madai Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa kwa shauri hilo ni lazima kuleta mashaidi wako/wenu na hati zote zinazo husu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Zingatia kama hukuhudhuria/ hamku hudhuria siku iliyo tajwa hapo juu na mahakama ikathibitisha kuwa umepokea /mmepokea kuitwa shauri hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo, tarehe 25/07/2020.

Hakimu mkazi mahakama ya mwanzo
KATORO GEITA

15794302

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ADOLF SIMONI MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye namba za usajili **MC 335 AWN** Chassis No. **MD2A21BZ5EWA71633,** Engine No. **PFZWEA33521.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/489049/2019.**

115793702

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW MWAKAPOLA KIMONGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 661 AYG** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/TAN/RB/493180/2020.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW MWAKAPOLA KIMONGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 319 ACK.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/TAN/RB/493054/2020.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo PONGWE TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 11/2020**

Ombi la **ELIAS TAKI KIGIGA** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **GASPA TAKI KIGIGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 13/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 15/06/2020.

MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

157941

---

## TANGAZO KUPOTEA KADI YA GARI

WANGU JOSEPH NDELEMI
MKAZI WA IGUNGA

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE JINA LA JUSTINE LUTULA NKYALU NAMBA ZA USAJILI T.950 APH TOYOTA- COROLLA YENYE RANGI YA SILVER CHASSIS NAMBA AE 1105138632 AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2020 MAENEO YA IGUNGA

YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA WANGU JOSEPH NDELEMI KWA SIMU NAMBA 0627334210

RB NAMBA IGU/RB/850/2020

215793302

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MAKOYE HUYA MAKELEMO**
anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili T.778 BCG aina ya SANLG Chassis namba LBRSPJB50990 13595, Engine namba C9963482.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi
MBE/MBE/RB/493433/2020.

215794202

---


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Majaji, mahakimu watetea haki za wanawake, watoto

**Na Futuna Seleman,** BAGAMOYO

CHAMA cha Mahakimu na majaji wanawake nchini (TAWJA), kimeshauri watoa uamuzi wa kisheria nchini kwa mashauri yanayohusu haki za binadamu na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wayatazame kwa jicho la kipekee.

Kimesema kuyapa nafasi kusaidia kuandaa taarifa za matukio hayo kwa usahihi.

Mwenyekiti wa chama hicho, Jaji Joaquine De-mello, aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tano kuhusu masuala ya haki za binadamu na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wilayani Mkoa wa Pwani.

Alisema takwimu zinahitajika ili kupata nguvu ya ziada kuyasimamia kikamilifu.

Jaji De-mello alisema kila mtoa haki mwanamke anajiunga na chama hicho, lengo ni kuwawezesha wenyewe kama watoa uamuzi uwezo katika utoaji haki za watoto na masuala ya ukatili wa kijinsia.

"Tumekuwa tukijiuliza na sisi jinsi ambavyo tunazidisha jitihada za kupambana, lakini taarifa zimekuwa nyingi, tunashukuru vyombo vya habari kusaidia watu wanaofanyiwa vitendo hivyo wanajitokeza," alisema Jaji De-mello.

Jaji De-mello alisema utafiti mbalimbali umegundua kuwa matukio mengi ya ukatili wa kijinsia yanatokea majumbani ndani ya familia kwa ndugu wa damu na kutolea mfano matukio ya kulawiti watoto kwa baba wazazi na kuwapa ujauzito.

"Taarifa zinaeleza chanzo cha matatizo hayo ingawa kuna upungufu katika mila ukosefu wa elimu kutokuwa na utayari wa kuyasimamia kuyazungumza na kuyapigia kelele," alisema Jaji De-mello.

Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Dk. Gerald Ndika, akizungumza kama mshiriki wa mafunzo hayo alisema matukio mengi ya ukatili yanasababishwa na mila potofu ukosefu wa elimi kwa jamii lakini alishauri tafsiri ya sheria kwa watoa uamuzi itumike kulingana na matukio ya mazingira yalivyo.

"Chanzo cha haya mambo ni matukio yanayosababishwa na mambo mengi mojawapo ikiwa ni mila potofu, uelewa ni mdogo, mtu mwingine anaona kumpiga mkewe ama mtoto wake ni haki yake," alisema.




Ofisa wa Benki ya NMB Tawi la Clock Tower mkoani Arusha, Mussa Lumala (kushoto), akimkabidhi nyaraka za bima mmoja wa wateja katika benki hiyo, Beatrice Sekela, baada ya kukata bima tawini hapo, jana. Habari Uk. 10. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kairuki ataka miundombinu kwa wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, ameiomba mikoa na halmashauri kutenga maeneo ya uwekezaji na kuyawekea miundombinu stahiki ili kuwavutia wawekezaji.

Alikuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuhitimisha ziara yake ya siku 5 katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya iliyomsaidia kujifunza, kujionea uwekezaji pamoja na kuzungumza na wawekezaji katika ukanda huo.

Alikipongeza Kituo cha Kuendeleza Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), kwa kuwa mfano mzuri katika kuhamasisha uwekezaji, na kutaka taasisi zingine kuiga mfano huo.

Waziri alisema mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ina fursa nyingi za uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwamo za utalii, kilimo na ufugaji.

Aliwahimiza wakuu wa mikoa na halmashauri kutenga maeneo ya uwekezaji na kuyawekea miundombinu stahiki ili kuendelea kuvutia wawekezaji nchini.

"Kila mkoa na halmashauri zake ni vizuri kutenga maeneo ya uwekezaji sambamba na kuweka miundombinu rafiki ili kuwatia moyo wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza nchini," alisema Waziri Kairuki.

Alisema serikali inaweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara na wawekezaji ili kuwavutia wawekezaji kufanya shughuli na kukuza la pato taifa.

Aliwataka wawekezaji kujisajili kwa hiari kwenye Kituo cha Uwekezaji Nchini (TIC) ili kunufaika na fursa zilizomo katika kituo hicho.

Mkurugenzi Mtendaji wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, alisema kituo kitaunganisha nguvu kutoka sekta za umma na binafsi ili kutoa mchango chanya katika maendeleo ya taifa.

## Familia yaomba msaada baada ya nyumba kuuzwa

**Na Elizabeth Zaya**

FAMILIA ya Aristide Ishebabi wa Sinza, jijini Dar es Salaam, imewaomba wasamaria wema kuwasaidia kupata mahali pa kuishi baada ya nyumba waliyokuwa wakiishi kupigwa mnada.

Akizungumza na waandishi wa habari, baba wa familia hiyo, Aristide Ishebabi, alisema tangu nyumba yao kupigwa mnada miaka minne iliyopita wanaishi nje na watoto na hivyo kuhatarisha maisha yao.

Ishebabi alisema nyumba yao ilikuwa namba 260 katika kitalu E, Sinza, Kinondoni.

"Ni miaka minne sasa tangu nyumba yetu ipigwe mnada, awali baada ya nyumba yetu kupigwa mnada tulipata wasamaria wema ambao walituhifadhi, lakini baadaye walisema hawawezi kutusaidia tena, kwa hiyo mpaka sasa tunalala na kupika nje kama unavyoona," alisema Ishebabi.

Akifafanua juu ya adha inayopata familia hiyo, Wakili Godwin Mwapongo alisema kinachohitajika kwa familia hiyo kwa sasa ni kusaidiwa kwa namna nyingine kwa sababu tayari nyumba yao imepigwa mnada na inamilikiwa na mtu mwingine.

## FADeV yawezesha wanawake migodini

**Na Sara Magesa,** GEITA

ADHA ya kuponda mawe kwa mikono na malipo ya ujira mdogo wanayoipata kinamama katika maeneo ya migodi ya dhahabu huwenda ikapungua baada ya taasisi isiyo ya kiserikali ya kuendeleza wachimbaji wadogo (FADev), kuanza mkakati wa kuwanunulia mitambo ya kusaga mawe inayotumia umeme.

Mbali na mitambo hiyo pia kinamama wanaendelezwa kwa kupatiwa elimu ya ujasiriamali wa kutengeneza sabuni ili kuinua uchumi kwa njia mbadala badala ya kutegemea kazi za vibarua zinazoathiri afya zao, huku zikiwa na malipo kidogo.

Meneja mradi na utafiti kutoka FADev, Evans Rubara, aliyasema hayo baada ya kutembelea migodi ya wachimbaji wadogo wa Msasa, Nyarugusu na Nyakagwe na kutoa elimu ya kujikinga na virusi vya corona.

Alisema utafiti mdogo waliofanya wamegundua kinamama wanapata wakati mgumu zaidi kwenye kazi ya kuponda mawe, huku ujira ukiwa mdogo.

"Tumezungumza na kinamama tukawaeleza tuwasaidie nini, wakaomba wapewe elimu ya kutengeneza sabuni hivyo tukatafuta mwalimu kutoka SIDO ambaye anawapa elimu ya ujasiriamali ya kutengeneza sabuni," alisema Rubara.




# SOLSKJAER AIPA CHANGAMOTO MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer anataka kuona kikosi cha Manchester United kikimaliza msimu wote uliobaki bila kufungwa mechi hata moja.

United wamecheza mechi 14 bila kufungwa wakati wakipambana kutafuta nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, huku wakiwa bado wapo kwenye michuano ya Ligi ya Europa na Kombe la FA.

Vijana wa Solskjaer, ambao wapo nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi, watacheza na Chelsea kwenye nusu fainali ya Kombe la FA, huku pia wakiwa kwenye wakati mzuri wa kufuzu robo fainali ya Kombe la Europa.

Kocha huyo wa United amewapa changamoto wachezaji wake kumaliza msimu huu bila kufungwa.

"Timu ya Manchester United inatakiwa kwenda katika kila mchezo na kuhakikisha wanaibuka na ushindi," alisema Solskjaer akiviambia vyombo vya habari vya Uingereza.

"Jibu rahisi (kama unakwenda bila kufungwa) ni sawa, lakini jibu gumu ni kama mambo yanakuwa tofauti na hilo.

"Bila shaka, vitu tofauti vinaweza kutokea kwenye mechi hizi, lakini tuna matumaini ya kuimarika na kuendeleza ushindi kadili inavyowezekana."

# Klopp hatarajii usajili mkubwa

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amekubali Liverpool haitakuwa na usajili wenye kelele wakati dirisha la majira ya joto litakapofunguliwa hivi karibuni, na hatarajii vinginevyo.

Liverpool ilitwaa taji lake la kwanza la Ligi Kuu England tangu mwaka 1990 msimu huu na wameshinda mechi 28 kati ya 31 za ligi hiyo.

Bado, Liverpool imekuwa ikihusishwa na uhamisho wa wachezaji kama nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, Kai Havertz wa Bayer Leverkusen na kiungo wa Bayern Munich, Thiago Alcantara.

Lakini Klopp amesema linaweza kuwa dirisha la usajili la kimya kwa Liverpool, huku mlipuko wa virusi vya corona ukiwa umeathiri mambo ya fedha kwa soka la dunia yote.

"Ni namna corona ilivyokuwa na athari kwenye uchumi wa klabu na maisha kwa ujumla.

"Sio tu soka, kwani wote tutatakiwa kulipa huduma za maisha yetu ya kila siku, hivyo mambo mengi yameathirika," alisema.





# *Rodgers 'amkingia kifua' Jamie Vardy*

**LONDON,** England

BRENDAN Rodgers ametetea kiwango cha, Jamie Vardy na kusema akili yake ilikuwa kwa timu yote ya Leicester City wakati huu wakiwa wanasuasua kufunga mabao.

Tangu kurudi kwenye Ligi Kuu England mapema mwezi uliopita, Leicester imefunga bao moja tu katika mechi tatu, na ilitolewa na Chelsea kwenye hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA baada ya kuchapwa 1-0, Jumapili.

Vardy hajafunga bao katika mechi zote tatu, lakini amefunga mabao 19 katika mechi 33 msimu huu, akiwa na pasi za mwisho sita.

Alipoulizwa kuhusu kiwango cha fowadi wake huyo, Rodgers alimtetea Vardy na kusema alitaka kiwango cha juu kwa safu yote ya ushambuliaji, sio tu kwa Mwingereza huyo.

"Wengi wanamfikiria zaidi Jamie, lakini hili halimhusu Jamie, hili ni jukumu la timu nzima na ni majukumu yangu kutafuta njia ambayo tunaweza kuongeza nafasi ya kufunga mabao," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni jukumu la kila mtu. Nafikiri kama unaangalia rekodi yake ya ufungaji mabao msimu huu na kile alichokifanya hadi sasa, hakuhitaji kujadiliwa sana, kwa sababu yeye ni mmaliziaji tu."

Leicester City, ambao wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo, leo Jumatano watakuwa ugenini kucheza na Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

## HABARI MICHEZO

# Kurzawa asaini mkataba mpya PSG

**PARISI,** Ufaransa

MLINZI wa Paris Saint-Germain, Layvin Kurzawa, atabakia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, baada ya kusaini mkataba mpya ambao unamweka hapo hadi mwaka 2024.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka mara tu mkataba wake utakapomalizika na alikuwa akitajwa kuwaniwa na miamba wa Ligi Kuu England, Chelsea na Arsenal.

Hata hivyo, wakati Thiago Silva, Edinson Cavani na Thomas Meunier wanaondoka pale Parc des Princes mwezi ujao, Kurzawa amekubali kuongeza mkataba na kikosi hicho cha Thomas Tuchel.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ameshinda mataji manne ya Ligue 1 katika misimu yake mitano ya kukaa na PSG, pamoja na Kombe la Ligi na Kombe la Ufaransa mara tatu.

Kurzawa, ameichezea Timu ya Taifa ya Ufaransa mechi 13, amecheza mechi 123 kwa PSG katika mashindano yote na kufunga mabao 13.

Juan Bernat amekuwa akicheza zaidi kama mlinzi wa kushoto kwa kikosi hicho cha Tuchel tangu msimu wa 2019/20, lakini kocha huyo mapema mwaka huu alisema "anamhitaji" pia Kurzawa.

Wakati msimu wa Ligue 1 ulimalizika Aprili kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, PSG – walipewa taji la ligi hiyo kwa sababu walikuwa wanaongoza kwa pointi nyingi kileleni.

PSG pia wapo kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, michuano ambayo itaendelea tena kuanzia Agosti mwaka huu, mjini Lisbon.






# BARCA YAMSAJILI RASMI PJANIC

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wamekubali kumsajili, Miralem Pjanic kutoka Juventus kwa ada ya awali ya euro milioni 60, huku Arthur akiwa amekubali kuhamia upande wa pili kwa kibibi kizee hicho cha Turin.

Pjanic atasaini mkataba wa miaka minne kuichezea Barca na atajiunga nao baada ya kukamilika kwa msimu huu 2019/20.

Mapema Jumatatu, mabingwa hao wa LaLiga walithibitisha kwamba Arthur atajiunga na Juve kuanzia msimu ujao kwa ada ya awali ya euro milioni 72.

Bianconeri hao bado hawajathibitisha na kutoa maelezo kuhusu mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil.

Mchezaji wa kimataifa wa Bosnia-Herzegovina, Pjanic amemzidi miaka saba Arthur na amekuwa pale Juve tangu alipotua akitokea AS Roma mwaka 2016.

Pjanic ameshinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, katika kila msimu kwa misimu mitatu pale Turin, akifunga mabao 22 katika mechi 171 alizoichezea klabu hiyo kwenye mashindano yote.

# *Timu ya Inzaghi kucheza Ligi Kuu*

**ROME,** Italia

TIMU ya Filippo Inzaghi, Benevento imepanda daraja na itacheza Ligi Kuu Italia, Serie A, Jumatatu huku mechi saba zikiwa bado hazijamalizika.

Straika wa zamani wa Cagliari, Marco Sau alitoka benchi na kufunga bao pekee kwenye mchezo huo wakati Benevento wakiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Juve Stabia, kwenye Ligi Daraja la Pili, Serie B.

Benevento, ambao wameshinda mechi 23 kati ya 31 za ligi huku wakiwa wamepoteza mchezo mmoja tu, wakiwa wanaongoza kwa zaidi ya pointi 24 kileleni.

Ascoli ilikuwa klabu ya mwisho kupanda huku zikiwa zimebakia mechi saba ligi kumalizika, na walifanya hivyo msimu wa 1977/78.

Benevento imetinga Ligi Kuu Italia kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka mitatu, lakini walishuka ndani ya msimu mmoja baada ya kupoteza mechi 14 mfululizo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEMANJA AMSHUKURU SOLSKJAER KUMWAMINI

## Mserbia huyo aeleza yeye ni 'askari' anayesubiri maagizo kutoka kwa kocha na...

**MANCHESTER,** England

NEMANJA Matic kamwe hajapoteza imani na uwezo wake katika kuaminiwa na Ole Gunnar Solskjaer na kupambania nafasi yake katika kikosi cha kwanza, pale Manchester United.

**Kiungo huyo amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Old Trafford baada ya kuwa na wakati mgumu wa kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara msimu huu, lakini sasa ameanza kuaminiwa.**

Matic, ambaye amejipambanua yeye mwenyewe kama "askari", amesisitiza mara zote alikuwa anajiunga mkono mwenyewe na kulazimisha kupata nafasi katika mipango ya Solskjaer.

"Mara zote nilijaribu kuwa mtulivu na kucheza kwa kiwango changu bora kabisa ninapokuwa dimbani, haijalishi kama katika mazoezi au kwenye mechi," amesema mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia, ambaye alijiunga na United akitokea Chelsea mwaka 2017, akiiambia Sky Sports.

"Tayari nimecheza soka kwa muda mrefu sana na hali hii ni ya kawaida, wakati mwingine huwezi kupata nafasi ya kucheza na kocha hakuoni kama wewe ni chaguo la kikosi cha kwanza. Unakubali hilo au unatakiwa kuwa mchezaji mwenye uelewa na kutulia.

"Unatakiwa kujituma, kusubiri kwa nafasi na ukipata hakikisha unaitumia. Hicho ndio pekee nilichokuwa nakifanya.

"Sasa hali ni tofauti, kocha anaaniamini mimi zaidi. Mimi ni askari na nasubiri maelekezo kutoka kwa timu yangu ya makocha.

"Kuwa mkweli, wakati ambao huchezi, bila shaka unafikiri kuhusu kila kitu, lakini kichwani mwangu mara zote nilijitahidi kuwa na mawazo chanya tu.

"Mara zote nilikuwa naamini kuhusu ubora wangu na najua kwamba nikifanya kazi kwa bidii nitaweza kupata nafasi ya kucheza tena na tena."

United imefanikiwa kutinga nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 katika muda wa ziada katika mchezo dhidi ya Norwich City uliochezwa Jumamosi iliyopita.

## ZISIKUPITE

### GREALISH KUMRITHI SANE

MANCHESTER City itamsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish (24), kama Bayern Munich itamnunua winga wake Mjerumani, Leroy Sane (24). Manchester United inatajwa pia kumwania Grealish. ***(Telegraph - subscription required)***

### GOMES ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inajipanga kumsajili kiungo wa Manchester United na Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 ( U-20), ya England, Angel Gomes, ambaye anawaniwa pia na klabu nyingine za Ulaya. ***(Independent)***

### MAURICIO ATAKIWA BENFICA

BENFICA inamtaka Kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino kuwa mwalimu wake mpya baada ya Bruno Lage kutangaza kujiuzulu kuifundisha timu hiyo. ***(TSF - in Portuguese)***

### DANI KUONDOKA ARSENAL

ARSENAL haitafanya tena mchakato wa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos (23), baada ya mkataba wake klabuni hapo kumalizika. Ceballos alisajiliwa akitokea Real Madrid. ***(Sun)***

### HAKIMI AIKATAA UNITED

BEKI wa kulia wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Morocco, Achraf Hakimi (21), ambaye yuko kwa mkopo Borussia Dortmund amekataa ofa iliyofika kwake kutoka kwa Manchester United. ***(AS, via Manchester Evening News)***

### KEANE ATAKIWA AZERBAIJAN

KIUNGO wa zamani wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland na Manchester United, Roy Keane yuko katika mazungumzo na Azerbaijan ili kuifundisha timu yao ya Taifa. ***(Sun)***

### NEWCASTLE, ARSENAL VITANI

NEWCASTLE United na Arsenal ni baadhi ya klabu za Ligi Kuu England ambazo zimeonyesha nia ya kumsajili straika wa Wolfsburg Mholanzi, Wout Weghorst (27), ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 31.9. ***(Bild - in German)***

### ROBERT KUTUA NEWCASTLE

MABOSI wa Newcastle United wanajiandaa kumsajili mshambuliaji Mfaransa, Thomas Robert (19), ambaye ni mtoto wa winga wake wa zamani, Laurent Robert. Mshambuliaji huyo anaichezea Montpellier lakini atasajiliwa kama mchezaji huru. ***(Mail)***

### PSG, KURZAWA WAMALIZANA

BEKI wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Layvin Kurzawa (27), ambaye alihusishwa kujiunga na Arsenal na Liverpool, amesaini mkataba mpya wa miaka minne na mabingwa hao wa Ligue 1. ***(Goal)***

### KLOPP ATOA MSIMAMO

MABINGWA wapya wa Ligi Kuu England, Liverpool haitatumia kiasi kikubwa cha "mamilioni na mamilioni" katika dirisha lijalo la usajili litakapofunguliwa, Jurgen Klopp, kocha wa timu hiyo amesema. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Mtibwa yakubali mambo magumu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mtibwa Sugar kwa mara ya kwanza imekiri iko katika hali ngumu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na inatakiwa 'ikaze msuli' ili ijiondoe kwenye janga la kushuka daraja.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, alisema jana msimu huu haukuwa mzuri kwao, lakini watajitahidi kwa kila hali, wakiwa na wachezaji wazuri pamoja na benchi la ufundi, hata hivyo imeshindikana na badala yake wamejikuta wakiwa kwenye hali hiyo.

"Tupo kwenye hali ngumu sana, miaka 25 tumekuwa kwenye ligi, lakini sitousahau mwaka huu au msimu huu wa 2019/20, tunapitia kipindi kigumu sana na hatujawahi kushika nafasi za chini kama hizi, lakini kuomba Mungu ili tusalie Ligi Kuu na tukifanikiwa, tutaanza kufanya marekebisho ya kikosi kwa msimu ujao," alisema Kifaru.

Alitangaza rasmi kuwa iwapo Mtibwa Sugar itashuka daraja, basi atastaafu nafasi yake katika klabu hiyo ya Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

"Kama itatokea bahati mbaya tukishuka, basi na mimi nitastaafu kazi hii, lakini kwa sasa tuna mechi mbili ngumu za ugenini huko Mwanza dhidi ya Alliance na Mbao, tutajitahidi kupata ushindi kwenye mechi hizi ili tuwe kwenye hali nzuri," Kifaru alisema.

Mtibwa iko katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 37 baada ya kucheza mechi 32, imeshinda mechi tisa, sare 10 na kufungwa mechi 13.

## Simba Queens yaendeleza dozi

**Na Saada Akida**

SIMBA Queens imeendelea kufanya vizuri katika Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania baada ya kuichapa Ruvuma Queens mabao 2-0, katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Majimaji mjini Songea.

Mabao ya Simba Queens katika mechi hiyo yalifungwa na Opa Clement na Mwanahamisi Omari 'Gaucho'.

Kwa matokeo hayo, Simba Queens imeendelea kujiimarisha kileleni kwa kufikisha pointi 32, ikifuatiwa na Alliance Girls yenye pointi 28 ambayo juzi ilifungwa mabao 2-1 na Kigoma Sisterz huku Ruvuma Queens yenye pointi 27 ikifuatia.

Mabingwa watetezi, JKT Queens wako katika nafasi ya nne wakiwa na pointi 26. Kocha wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema hesabu zake ni kuona anashinda mechi zilizobaki ili kujiimarisha kutwaa taji la ubingwa msimu huu ikiwa ni mara ya kwanza.

Mgosi alisema baada ya kupata ushindi dhidi ya Ruvuma Queens, na kuona mapungufu yao sasa anaendelea kuwaimarisha zaidi wachezaji wake ili kupata matokeo chanya katika mchezo unaofuata dhidi ya Panama Girls.

"Msimu huu tumedhamiria kutwaa ubingwa, tunajipanga vizuri kuhakikisha tunapata pointi muhimu kwa kushinda mechi zetu zote ikiwamo Panama na baadaye tutawafuta JKT Queens," alisema Mgosi.

# KLABU 4 UWANJANI LIGI KUU ZANZIBAR IKIREJEA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KINYANG'ANYIRO cha kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kinatarajiwa kurejea tena kuanzia leo kwa Zimamoto kuwakaribisha Mlandege katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa kwenye Uwanja wa Mau A.

**Ligi hiyo inaendelea baada ya kusimama kwa zaidi ya miezi mitatu kutokana na kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona na leo mechi nne zitachezwa katika vituo viwili vya Unguja na Pemba.**

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Maafande wa JKU watakaovaana na kikosi cha Jeshi la Wananchi Tanzania, Kipanga kwenye Uwanja wa Mau B, kuanzia saa 10: 00 jioni.

Katika kituo cha Pemba kwenye Uwanja wa Gombani, mwenyeji Selem View ataikaribisha Mafunzo ya Unguja kuanzia saa 8:00 mchana na baadaye jioni, Jamhuri itachuana na Polisi kwenye uwanja huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada Vuai, alisema hadi kufikia sasa maandalizi yote kuhusiana na mwongozo wa afya kama yalivyotolewa na serikali ili kujikinga na corona yamekamilika.

Vuai alisema kuwa timu zote zimepewa mwongozo huo na mwingine uliotolewa na ZFF katika jitihada za kujikinga na virusi vya corona visiwani hapa.

"Hadi kufikia sasa maandalizi yote yanakwenda vizuri, tumetoa mwongozo ya afya kwa timu zote za Ligi Kuu na wahudumu wote ambao wanasimamia mechi, ZFF inafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Michezo pamoja na Wizara ya Afya katika utekelezaji wa yale yote ambayo serikali imeyaagiza," Vuai alisema.

Kiongozi huyo alizitaka timu zote kutoongozana na mashabiki wao wakati wanaingia viwanjani ili kutii amri iliyotolewa wakati ligi hiyo inaruhusiwa kuendelea tena kwa lengo la kukamilisha msimu.




Beki wa DTB FC, Omary Kunambi (kushoto), akimkabili mshambuliaji wa Tukuyu Stars katika mechi ya Ligi Daraja la Pili Kundi C iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi. DTB ilishinda magoli 2- 1 kufuzu kucheza hatua ya Sita Bora ya ligi hiyo itakayofanyika Ruangwa, Lindi kuanzia Julai 4, mwaka huu. **PICHA: DTB FC**

# Mhilu aiita Yanga SC mezani

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Kagera Sugar, Yusuph Mhilu amesema anazikaribisha mezani klabu mbalimbali za Ligi Kuu Bara zinazohitaji huduma yake, lakini akiipa nafasi kubwa timu yake ya Kagera Sugar.

Mhilu, ambaye ni mchezaji wa zamani wa Yanga ambaye msimu huu alisaini mkataba wa mwaka mmoja akitokea Ndanda FC, alisema kuwa anamaliza mkataba wake hivi karibuni na timu yoyote yenye ofa nzuri ndiyo atakayokubali.

"Timu yoyote ile naikaribisha tuzungumze nayo, nipo tayari kuichezea timu yoyote hata Yanga, timu yangu ya zamani, ili mradi tu nikubaliane na kile ambacho watanipatia, lakini nafasi ya kwanza kabisa nitaipa timu yangu ya sasa (Kagera Sugar), kwa sababu mpaka sasa mimi bado ni mchezaji wao," alisema Mhilu.

Mchezaji huyo amekuwa kwenye kiwango bora kabisa msimu huu, baada ya kufikisha magoli 13, akishika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji, nyuma ya Meddie Kagere wa Simba ambaye amepachika wavuni mabao 19.

"Kikubwa ni kujituma na kujiwekea malengo, ndiyo maana unaniona hata niliporejea kutoka kwenye mapumziko ya corona, kiwango changu bado hakijaporomoka na nikipata nafasi za kufunga nazitumia," alisema winga huyo.

Alisema lengo lake msimu huu ni kufikisha magoli 20, hivyo amebakisha magoli saba tu ili kutimiza lengo.

Katika mechi ya Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Mhilu alifunga bao kwenye mechi dhidi ya KMC iliyoisha kwa sare ya bao 1-1, huku akifunga bao pekee Jumatano iliyopita walipoikaribisha Azam FC.

# Michezo

Jumatano Julai 1, 2020

Nipashe




Nemanja amshukuru Solskjaer UKURASA 22



Straika wa Arsenal, Alexandre Lacazette (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Sheffield United, Chris Basham katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Kombe la FA England iliyochezwa juzi usiku. Arsenal ilishinda mabao 2-1. **PICHA : MTANDAO**

## Morrison adaiwa kukimbilia Sauzi

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Yanga, Bernard Morrison anadaiwa kuondoka nchini na kuelekea Afrika Kusini bila ya kupata ruhusa kutoka kwa uongozi wa klabu yake, imefahamika.

Taarifa zilizopatika jijini Dar es Salaam jana zinasema Morrison alitoroka katika kambi ya timu hiyo tangu juzi usiku, wakati akiwa ni sehemu ya mipango ya kikosi cha kilichoivaa Kagera Sugar jana usiku.

Chanzo chetu kiliendelea kusema nyota huyo alitofautiana na viongozi wa timu waliokuwapo kambini baada ya kukataliwa kuondoka.

“Ni kweli hayupo kazini, alitoroka kambini, ameondoka kwa mabavu, kuna mambo mengi yanaendelea kumhusu mchezaji huyo,” kiliongeza chanzo chetu.

Nyota huyo ambaye alifunga bao pekee katika mchezo wa watani wa jadi Machi 8, mwaka huu, aliendelea kutokuwa na mahusiano mazuri na viongozi wake baada ya kutakaa kuvunja mkataba mpya wa miaka miwili ambao alisaini hivi karibuni.

# Simba, Azam zaidi ya heshima

**Na Somoe Ng'itu**

●●● Zinakutana katika mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la FA, zikitambiana...

HAKUNA kulala! Ni pale mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba watakapowakabili Azam FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa leo kuanzia 1: 00 usiku kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Azam FC ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo ambayo hutoa tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Simba itashuka dimbani leo tayari ikiwa na tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikiwa na mechi sita mkononi za kumaliza msimu wa 2019/20, huku Azam FC yenyewe zikipambana na Yanga kumaliza kwenye nafasi ya pili.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema kikosi chake kiko tayari na mechi ya leo na wamejipanga kuendelea kupambana ili kutimiza malengo ya kukinyakua kikombe cha mashindano hayo.

Sven alisema anafahamu mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani, lakini amewaandaa wachezaji wake kucheza katika kiwango bora kwa sababu Azam FC pia ni timu nzuri na yenye wachezaji wazoefu.

“Tunachokiangalia ni kufanya vizuri, mechi haitakuwa rahisi, lakini tunacheza na timu ambayo kila kitu chake kinategemea michuano hii, kwa kifupi tuko tayari kwa mapambano,” alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Aliongeza baada ya kumaliza kukamilisha malengo namba moja, nguvu zao wamezielekeza kwenye michuano hii ambayo msimu huu wanahitaji kuweka rekodi nzuri na si kutolewa mapema.

Naye Kocha Mkuu wa Azam FC, Aristica Cioaba, alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana na kuhakikisha wanashinda mechi hiyo ili wasonge mbele katika michuano hiyo.

“Ni mechi kubwa, kimahesabu tayari Simba ni mabingwa, nawapongeza pia kwa kutwaa ubingwa, wana wachezaji wazuri na kila nafasi ina wachezaji wawili wazuri, lakini kesho (leo), naamini haitakuwa siku yao, tutaingia uwanjani kwa lengo la kushinda,” alisema Cioaba.

Alieleza leo wachezaji wake wanatakiwa kucheza soka la kuvutia, wachezaji wake kuelewana na kuwa na ari ya juu na kuongeza umakini kila watakapokuwa na mpira.

“Wanatakiwa kujitoa zaidi, kwa sababu ni mchezo ambao timu moja itatoka na timu nyingine itaendelea na mashindano, najua kesho (leo), ni siku muhimu na ninawakumbusha wachezaji wangu kuongeza umakini katika kufunga, huu ndio ujumbe kwa mastraika wangu,” alisema kocha huyo.

Kiungo wa timu hiyo, Frank Domayo, aliiambia gazeti hili mechi ya leo itakuwa ngumu kwa pande zote, lakini wao watashuka dimbani kupambana kusaka ushindi.

“Simba ni timu ngumu, inawachezaji wazuri, kila kitu kiko sawa, na sisi pia tuna nafasi, kikubwa ni kupambana kuwania pointi tatu, kikosi kiko imara, tumekaa pamoja kama wachezaji na kuelezana malengo yetu, “ Domayo alisema.

Simba itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Azam FC, ambayo leo itaendelea kuwakosa nyota wake wa kimataifa kutoka Ghana, akiwamo golikipa Razack Abalora.

Robo fainali nyingine ya michuano hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Sahare All Stars ya jijini Tanga dhidi ya Ndanda FC kutoka mkoani Mtwara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >